

MASHAIRI YA KIJAMII

الأشعار الإجتماعية

Kimetungwa na:

Juma S. N. Mgambilwa

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 – 9987 – 17 – 034 – 0

Kimetungwa na:
Juma S. N. Mgambilwa

Kimehaririwa na:
Al-Haj Ramadhani S. K. Shemahimbo

Kimepitwa na:
Mbarak Ali Tila

Kimepangwa katika Kompyuta na:
Al-Itrah Foundation

Toleo la kwanza: Septemba, 2015
Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
Tovuti: www.ibn-tv-com
Katika mtandao: www.alitrah.info

YALIYOMO

Neno la Mchapishaji	vi
1. Hapa tulipo	1
2. Tuwasaidiye hawa	1
3. Nawapenda Albino	2
4. Usalama barabarani	3
5. Msimwage damu	4
6. Heshima kwa wazazi	5
7. Tuchape kazi	6
8. Okoa kizazi kipyta	6
9. Mtu wa kwanza ni mwalimu	7
10. Sayari ya kielimu	8
11. Fungeni ndowa	9
12. Tufanye tunayosema	10
13. Kuhusu Mwenyezi	11
14. Maumivu ya husuda	11
15. Utamu wa kusengenyana	12
16. Kiburi si maungwana	13
17. Utapeli	14
18. Kiwanda cha unafiki	15
19. Dhana mbaya	15
20. Kisirani	16
21. Hofu	16
22. Vuno la mtu mwoga	17
23. Wizi na Ujambazi	18
24. Hiyana	19

25. Shimo la hatari zinaa	20
26. Uongo	20
27. Upendo kwa vitendo	21
28. Mizozo ya nini?.....	22
29. Usilalamike jipange	23
30. Huruma ni utu wema	24
31. Utaweza uongozi	25
32. Ukihamaki	25
33. Usiwe ndumilakuwili	26
34. Kuhemkwa na ukali	27
35. Kubweteka	28
36. Samehe upate raha	29
37. Tuwe wabunifu	29
38. Kuzama kwa meli	30
39. Mafuriko yafikapo	32
40. Mabomu Gongo la mboto	32
41. Usiwe na pupa	33
42. Mwenye dini	34
43. Wacha jazba	35
44. Tuepuke dhuluma	35
45. Haki za wanawake	36
46. Akigoma Daktari	37
47. Madhara ya Ulevi	38
48. Usiwe kupe	39
49. Madhara ya rushwa	40
50. Ukabila na udini.....	40

NENO LA MCHAPISHAJI

Mashairi ni sanaa muhimu sana katika jamii, katika kufikisha ujumbe wa aina mbalimbali, katika kuipa jamii taarifa zinazojiri ndani ya jamii yao, na katika jumuiya zao na ulimwenguni kwa ujumla. Ni kwa kupitia sanaa hii jamii huhamasishwa kushiriki katika masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo yao na ya nchi yao. Halikadhalika sanaa hii ni burudani maridhawa katika jamii inayohusika.

Katika kitabu hiki tunawaletea wasomaji wetu mashairi yaliyotungwa na malenga wetu, Ndugu Juma S. N. Mgambilwa.

Katika kitabu hiki mshairi ameandika kuhusu kadhia mbalimbali zilizotokea hapa nchini, k.v. ustawi wa jamii, vijana, uongozi, uadilifu wa viongozi, tabia njema n.k. Ameshughulikia jumla ya mada 50.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa makubwa, husasan wakati huu ambapo jamii nyingi ikiwemo ya kwetu zinashuhudia uporomokaji mkubwa wa maadili

Tunamshukuru ndugu yetu mtunzi wa mashari haya kwa kazi kubwa aliyofanya ya kuandika na kuyakusanya mashairi haya katika kitabu hiki mlichonacho mikononi mwetu. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duni-ani na kesho Akhera pia. Amin!

**Mchapishaji
Al-Itrah Foundation**

1. HAPA TULIPO

1. Kwa jina Rahmani, kila kitu naanzia
Tumwa apate amani, na kizazi, chake pia
Nimekuja na maoni, viumbe yana wafaa
Jiulize wewe nani, upate kujitambua.
2. Kwa pamoja tuliyeni tupate kuyachambua
Swali nawaulizeni lanihusu mimi pia
Tulijibu kwa makini, tuyapate manufaa
Jiulize wewe nani, upate kujitambua
3. Ndugu yangu wewe nani, ni wapi unatokea
Sasa upo duniani, ni kipi umekijia
Ukitoka duniani, wapi unaelekeea
Jiulize wewe nani, upate kujitambua
4. Kabla ya duniani, waweza kudokezea
Uliishi nyumba gani, na nguo ulizovaa
Ulifanya kazi gani, riziki kujipatia
Jiulize wewe nani, upate kujitambua
5. Nakuona duniani mwenyeji umezowea
Ulifika duniani, kwake umepachagua
Ukifika duniani, ni kwake utafikia
Jiulize wewe nani upate kuji tambua
6. Kawaida ya mgeni, safari ajiandaa
Masurufu mifukoni, ugenini kufikia
Wewe ulibeba nini, ukaja kwenye dunia
Jiulize wewe nani, upate kujitambua
7. Ni kwa usafiri gani, mwenzetu umetumia
Kuna masilahi gani, katika hii dunia
utarejea kwa nani, baada hii dunia
Jiulize wewe nani upate kujitambua.
8. Nauliza wewe nani, unayeniangalia
wengine hamnioni, lakini mwanisikia
mlipanga siku gani, kuja katika dunia
Jiulize wewe nani, upate kujitambua.
9. Mwatafuta kitu gani, katika hii dunia
Kiwafae maishani, na mkihama dunia

Sina shaka mwaamini, tutaihama dunia
Jiulize wewe nani , upate kujitambua.

10. wengine wanaamini, lengo la hii dunia
Nikushiba matumboni, kuoa na kuolewa
Hata nguruwe na nyani, waishi maisha haya
Jiulize wewe nani upate kujitambua.
11. Wengine wanatamani, kuimiliki dunia
Kudhulumu maskini, mayatima na wakiwa
Wakidhani duniani, maisha wayapatia
Jiulize wewe nani, upate kujitambua
12. Majumba yenyeye thamani, na mashamba
mengi pia
Kinafuatia nini, baada ya yote haya
Lengo lako lengo gani, ukiitoka dunia
Jiulize wewe nani, upate kujitambua
13. Vyakula vyako ghalani, ulivyojirundikia
Wamekushinda thamani, tembo na
pundamilia
Majani yote mbugani, washiba na kucheua
Jiulize wewe nani, upate kujitambua.
14. Wandugu jitafuteni, lengo ni kujitambua
Tumezidi kwa thamani, kila kitu cha dunia
Nawaaga kwa herini, beti hii naishia.
Jiulize wewe nani, upate kujitambua

2. TUWASAI DIE HAWA

1. Ndugu zangu hamjambo,wote nawasalimia
Tuyarekebishe mambo, Mungu akitujaalia
Dunia ni kama chombo, baharini chaelea
Kuliko kula makombo, bora kuwapakulia
2. Likilia la mgambo, lafaa kukimbilia
Usifuate mkumbo, wa wanopuuzia
Waweza kukosa mambo, yaletayo manufaa
Kuliko kula makombo, bora kuwapakulia

MASHAIRI YA KIJAMII

3. Nataka kusema jambo, kwa waliohudhuria
Litangazwe hadi ng' ambo, kila pembe ya
dunia
Kila mshibisha tumbo, akumbuke wenyenjaa
Kuliko kula makombo, bora kuwapakulia
4. Ukweli wa hili jambo, wengi linatuelea
Tunayaona makombo, mapipani yamejaa
Kwenye mifuko ya Rambo,
yemezagaazagaa
Kuliko kula makombo, bora kuwapakulia
5. Baada ya kushiba tumbo, ukatupa
kwenye jaa
Wayatamani makombo, masikini wenyenjaa
Nyumba zao ni machimbo, wengine
kwenye majaa
Kuliko kula makombo, bora kuwapakulia
6. Ile mifuko ya Rambo, ulotupa kwenye jaa
Mafukara ndiyo vyombo, vyakula
wanawekea
Yale makopo ya kimbo, huokota kwenye jaa
Kuliko kula makombo, bora kuwapakulia
7. Mboga yao utumbo, wa samaki na dagaa
Usiku wabeba Rambo, matambara yamejaa
Ukipita kwenye chombo, wawezekujionea
Kuliko kula makombo, bora kuwapakulia
8. Utashuhudia mambo, giza likishaingia
Utawaona mgambo, watakavyowatimu
Wataipata hujambo, walinzi wakisinzia
Kuliko kula makombo, bora kuwapakulia
9. Wakiumwa na matumbo, ili kujisaidia
Kwenye mfuko ya Rambo, haja zao zaishia
Yale makopo ya kimbo, wanywea na
kunawia
Kuliko kula makombo, bora kuwapakulia
10. Kuna wengine mgambo, wabaya
kupindukia,
Wanawafanya majambo, giza linapoingia)
Kila mgombea jimbo, alenge kuwakomboa,
Kuliko kula makombo, bora kuwapakulia
11. Nalisisitizia jambo, hili silakuachia
Watuhawa kwa maumbo, tunafanana
tambua
Mungukawapa maumbo, kama adamu na
hawa
Kuliko kula makombo, bora kuwapakulia.
12. Limelia la mgambo, ujumbe nawaachia
Tukomeshe haya mambo, bila hata kukawia
Wanetu wasoma ng'ambo, je wa mitaani
hawa?
Kuliko kula makombo, bora kuwapakulia.
13. Tusibakize makombo, tupike kwa kupimia
Hayatabaki makombo, yatupwayo kwenye
jaa
Israfu ndio jambo, ambalo twazuilia
Kuliko kula makombo, bora kuwapakulia.
14. Tusifuate mkumbo, wa vituko vya ulaya
Kuyahudumia mambo, yanayotia kinyaa
Mashindano ya urembo, si bora kushabikia
Kuliko kula makombo, bora kuwapakulia.
15. Nimezungumza mambo, wengi mnayaelewa
Mambo yakienda kombo, sote tutalaumiwa
Ili kufupisha mambo, beti hii naishia
Kuliko kula makombo, bora kuwapakulia.

3. NAWAPENDA ALBINO

1. Mungu ni mpole mno, jina lake nanzia
Ili aunge mkono, nitakayoelezea
Ndugu zetu Albino, na thamani yao pia
Tuwalinde Albino, wasije kuhujumiwa

MASHAIRI YA KIJAMII

2. Ndugu zetu Albino, ni viumbe wa dunia
Rangi zao za manjano, mwenzenu zanivutia
Kamwe siungi mkono, wanaowashambulia
Tuwalinde Albino, wasije kuhujumiwa
3. Ngozi zao Albino, nyepesi kupindukia
Nawahurumia mno, kwenye mionzi ya juu
Macho hayana maono, na ngozi kubabuliwa
Tuwalinde Albino, wasije kuhujumiwa
4. Natamani Albino, Masomo kuwapatia
Wapate ajira nono, Kivilini kufanyia
Nchi kupata mavuno, kodi zao kupatia
Tuwalinde Albino, wasije kuhujumiwa
5. Wenye laana kubwa mno, ni wanaowavizia
Ili kukata mikono, miguu shingo na pua
Siwapati mfano, viumbe wabaya hawa
Tuwalinde Albino, wasije kuhujumiwa
6. Nasikia minong'ono, kuna waliogundua
Viungo vya Albino, vinatengenezwa dawa
Kuleta uwezekano, wa kuwa bilionea
Tuwalinde Albino, wasije kuhujumiwa
7. Ni uongo wa maneno, mimi nawakatalia
Viungo vya Albino, si mali wala si dawa
Ndugu zetu Albino, wapo kila familia
Tuwalinde Albino, wasije kuhujumiwa
8. Na pia kuna maneno, vigezo yanatolewa
Kaburi la Albino, hawajalishuhudia
Mimi siungi mkono, maswali mabovu haya
Tuwalinde Albino, wasije kuhujumiwa
9. Makaburi mengi mno, nimeyashudilia
Mazishi ya Albino, niliyoyahudhuria
Wanadanganyika mno, wavivu kufikiria
Tuwalinde Albino, wasije kuhujumiwa
10. Kazi ziko nyingi mno, akili tukitumia
Utajiri mwangi mno, uchumi kujipatia
Kipi cha zaidi mno, ukifariki dunia
Tuwalinde Albino, wasije kuhujumiwa
11. Nami nauliza neno, kwa viumbe wa dunia
Ukishadhulumu mno, ukawa bilionea
Kipi cha zaidi mno, ukifariki dunia?
Tuwalinde Albino, wasije kujumiwa
12. Tuwalinde Albino, bado nasisitizia
Tupate uelewano, na muumba wetu pia
Nayafupisha maneno, beti hii naishia
Tuwalinde Albino, wasije kuhujumiwa

4. USALAMA BARABARANI

1. Kwa jina lake Jalali, shairi nawaleta
Namsalimu Rasuli, na watoto wake pia
Nimekuja na maswali, yafaa kuzingatia
Dereva kinga ajali, na wewe mwenda na njia.
2. Mwanadamu na ajali, siajabu kutokea
Lakini tatizo hili, uzembe unachangia
Sasa kwa kila mahali, watu wanateketea
Dereva kinga ajali, na wewe mwenda na njia.
3. Madereva wa malori, na wale wa daladala
Mnaendesha magari, usingizi mmelala
Mwauacha mstari, kuparamia jalala
Dereva kinga ajali, na wewe mwenda na njia.
4. Usingizi nao mali, yafaa kujipangia
Kaupumzishe mwili, kitandani kuingia
Ukiutuliza mwili, na akili hutulia
Dereva kinga ajali, na wewe mwenda na njia.
5. Wengi hufanya ajali, kwa sababu wamelewa
Usalama hawajali, Radio kufungulia
Honi za wenye magari, hawawezi kusikia
Dereva kinga ajali, na wewe mwenda na njia.

MASHAIRI YA KIJAMII

6. Kwa sababu ya ajali, wengi wameteketea
Tabia tuzibadili, tuweze kujiokoa
Ulevi tuache mbali, hautatusaidia
Dereva kinga ajali, na wewe mwenda na njia.
7. Kuna tatizo la pili, janga limetuvamia
Zapatikana ajali, Pikipiki kuititia
Ukifika Muhimbili, majeruhi wamejaa
Dereva kinga ajali, nawewe mwenda na njia.
8. Tuziepuke ajali, wengi zimesha waua
Wakitoka Muhimbili, viungo vimelemaa
Lanisikitisha hili, madereva na wambia
Dereva kinga ajali, na wewe mwenda na njia.
9. Barabara sipahali, pakuchezza chezea
Tuzitulize akili, mwili na mawazo pia
Tutafikiya mahali, ajali zitapungua
Dereva kinga ajali, na wewe mwenda na njia.
10. Dereva stahimili, kukubali kuchelewa
Kwa wenyenye mwendo mkali wapishe wende na njia
Huo siyo udhalili, bali ndiyo ushujaa.
Dereva kinga ajali, na wewe mwenda na njia.
11. Gari na mwendo mkali, hatari kwa abiria
Wa miguu tuwajali, Wanapokatisha njia
Na watoto wa skuli, vilema pia vichaa
Dereva kinga ajali, nawewe mwenda na njia.
12. Napenda adhabu kali, kwa madereva
wabaya
Tutaweza kubadili, ajali zilizo mbaya
Baada hii kauli, batili ninaishia
Dereva kinga ajali, na wewe mwenda na njia.

5. MSIMWAGE DAMU

1. Enyi wanawe Adamu, Mama yenu bibi Hawa
Nawatolea salamu, furaha imenijaa
Leo nimepata hamu, kuja kuwashutubia
Njia ya kumwaga damu, haitatusaidia
2. Mkiitwa wanadamu, nyote mnaitikia
Hakuna wakulaumu, wala anayekataa
Nyote ni ndugu wa damu, wazazi wenu ni hawa
Njia ya kumwaga damu, haitatusaidia
3. Mnanini wanadamu, dunia mwaichafua
Kwa kufyatua mabomu, na kuichafua hewa
Kwa wingi mwamwaga damu, kila pembe ya dunia
Njia ya kumwaga damu, haitatusaidiaa
4. Elewa mwanaadamu, hapa ulipofikia
Unamuudhi Adamu, na mkewe bibi Hawa
Ni ndugu zako wa damu, wote unaowaua
Njia ya kumwaga damu, haitatusaidia
5. Kupishana wanadamu, mawazo ni sawasawa
Ukipenda kunywa ndimu, mwingine anywa kahawa
Tende ukiona tamu, mwingine aona mbaya
Njia ya kumwaga damu, haitatusaidia
6. Wajibu haki nidhamu, vitu vyta kuvifidia
Kila mtu ni Hakimu wa nafsi yake pia
Akitaka kudhulumu, aweze kujizua
Njia ya kumwaga damu, haitatusaidia
7. Vita vyote vinadumu, katika hii dunia
Kujiona mwanadamu, yeche ndiye anafaa
Viumbe kuwashukumu, japo kwa kuwaonea
Njia ya kumwaga damu, haitatusaidia
8. Leo akija Adamu, na Hawa watashangaa

MASHAIRI YA KIJAMII

- Kuwaona wanadamu , wanauwana vibaya
Mwingine kameza bomu, sokoni kujilipua
Njia ya kumwaga damu, haitatusaidia
9. Mwingine ana mabomu, Manuwari zimejaa
Anasubiri msimu, aanze kuyalipua
Nawaonya wanadamu, mwendo huo si
sawia
Njia ya kumwaga damu, haitatusaidiaa
10. Mimi ninachofahamu mabaraza ya dunia
Wengine ni waalimu, mwaifundisha sheria
Wapi mwapata ugumu, dunia kuweka sawa
Njia ya kumwaga damu, haitatusaidiaa
11. Pamoja na ualimu, naamini mwakosea
Haki ya mtu ni ngumu, hasa ikipinduliwa
Hata kama hafahamu, maneno kupangilia
Njia ya kumwaga damu, haitatusaidia
12. Ndugu zangu wanadamu, tumeumbiwa
dunia
Tunapozimwaga damu, huko ni kuichafua
Haki wajibu nidhamu, ni vitu vyta kufidia
Njia ya kumwaga damu, haitatusaidia
13. Kuna maisha matamu, katika hii dunia
Bila ya kumwaga damu, haki ifuwate njia
Kufika hii sehemu, kwaherini nyote pia
Njia ya kumwaga damu, haitatusaidia
3. Ni hawa hawa wazazi, anasa walijinyima
Kuhakikisha malezi, yetu yanaenda vyema
Walituvisha mavazi, jamani baba na mama
Tuwaheshimu wazazi, tupate maisha mema.
4. Tulipofanya makazi, katika tumbo la mama
Baba akifanya kazi, kumuhudumia mama
Tumeishi kwa miezi, tisa tumboni mwa
mama
Tuwaheshimu wazazi, tupate maisha mema.
5. Sasa mama hajiwezi, kazi zake zimekwama
Akiletewa viazi, hataki ataka nyama
Nyama asema siwezi, bila uji wa mtama
Tuwaheshimu wazazi, tupate maisha mema
6. Ikifikia miezi, anatapa tapa mama
Amsubiri Mwenyezi, amletee rehema
Miguu ikifa ganzi, mama anahemahema
Tuwaheshimu wazazi, tupate maisha mema
7. Kwa mapenzi ya Mwenyezi, akajifungua
mama
Sasa kazi ya malezi, nayo ikamuandama
Kula chochote huwezi, wanyonya titi la
mama
Tuwaheshimu wazazi, tupate maisha mema
8. Kwenda chooni huwezi unamchafua mama
Makamasi na machozi, wampangusia mama
Umeshaweka makazi, kwenye mapaja ya
mama
Tuwaheshimu wazazi, tupate maisha mema

6. HESHIMA KWA WAZAZI

1. Namshukuru Mwenyezi, anayetupa uzima
Kurahisisha mapenzi, toka kwa baba na
mama
Tukayapata malezi, Mola kafanya hekima
Tuwaheshimu wazazi, tupate maisha mema
2. Tuwashukuru wazazi, hao ni baba na mama
Kutupatia malezi, hawakujali gharama
Hivyo walichapa kazi, kuhakikisha twasoma
Tuwaheshimu wazazi, tupate maisha mema
9. Ilipopita miezi, ukaanza kusimama
Pua limaja Inzi, umemtoroka mama
Mama kulala hawezi, chooni usije zama
Tuwaheshimu wazazi, tupate maisha mema
10. Ilipopita miezi, ukajifunza kusema
Kujieleza huwezi, maji unaita mma
Mama kajaa michuzi, meza umeisukuma
Tuwaheshimu wazazi, tupate maisha mema

MASHAIRI YA KIJAMII

11. Ukawa ni mwanafunzi, chekechea unasoma
Nguo kufua huwezi, bado ni kazi ya mama
Hadi kuwa mwanafunzi, kwenye vyuo
ukisoma.
Tuwaheshimu wazazi, tupate maisha mema
12. Sasa ni mkurugenzi, unamdharaun mama
Unamuona mshenzi, mjinga asiyesoma
Hayo makosa ya wazi, huko mbele
utakwama.
Tuwaheshimu wazazi, tupate maisha mema
13. Nawaonya kwa mapenzi, kuhusu baba na
mama
Magambilwa ni mtunzi, na Amina ndiye
mama
Saidi baba mzazi, hadi hapa nasimama
Tuwaheshimu wazazi, tupate maisha mema
5. Bwana fedha na mlinzi, wote ni watu wa
maana
Mmoja akinga wizi, mali ibaki salama
Bwana fedha ni mlinzi, fedha ibaki salama
Ndugu tuchapeni kazi, bila ya kuchukiana
6. Mgawanyiko wa kazi, ukitekelezwa vyema
Kwa moyo wenye mapenzi, kazi yote ni
salama
Ndipo utaona kazi, itakapoleta neema
Ndugu tuchapeni kazi, bila ya kuchukiana
7. Migongano kwenye kazi, haileti usalama
Unapoifanya kazi, ifanye kwa nia njema
Nimewawekea wazi, hadi hapa na simama
Ndugu tuchapeni kazi, bila ya kuchukiana.

7. NIDHAMU KATIKA KAZI

1. Habari gani wapenzi, kwa mabibi na
mabwana
Katuwezesha Mwenyezi, mpaka tumekutana
Kutafuta ufumbuzi wa yale mambo ya
maana
Ndugu tuchapeni kazi, bila ya kuchukiana
2. Maisha bila ya kazi, hayawezi yakafana
Kila mahala pa kazi, nidhamu muhimu sana
Kuanzia viongozi, na wale wa chini sana.
Ndugu tuchapeni kazi, bila ya kuchukiana
3. Karani na mpagazi, wote ni watu wa maana
Wote wakifanya kazi, bila kukejeliana
Wakifanya kwa mapenzi, na tija kupatikana
Ndugu tuchapeni kazi, bila ya kuchukiana
4. Kupiga deki ni kazi, iliyo muhimu sana
Bosi na mkurugenzi, mlizingatie sana
Ikiachwa hii kazi, Ofisi haina maana
Ndugu tuchapeni kazi, bila ya kuchukiana

8. OKOA KIZAZI KIPYA

1. Kumshukuru Mwenyezi, ni muhimu bila
shaka
Kwa wazazi na walezi, kuwausia nataka
Umuhimu wa malezi, mazuri yalonyooka
Vijana wa siku hizi, mbioni kuharibika.
2. Nikikumbuka malezi, hapa kwetu Afrika,
Kuzingatia mavazi, na vitendo kadhalika
Babu zetu tangu enzi, mafunzo waliyashika
Vijana wa siku hizi, mbioni kuharibika.
3. Wavulana hawawezi, nywele zao kuzisuka
Wasichana hawawezi, nguo fupi kujivika
Vijana leo mavazi, siyo ya kueleweka
Vijana wa siku hizi, mbioni kuharibika.
4. Kupambanua huwezi, yupi dada yupi kaka,
Wafanana kwa mavazi, wote nywele
wamesuka,
Wote mabega ya wazi, Hereni wamejivika
Vijana wa siku hizi, mbioni kuharibika.
5. Jamani haya malezi, ni wapi yanakotoka,
Sisemi utandawazi, uliotuzunguka

MASHAIRI YA KIJAMII

Haya ni maambukizi, ya nchi za Amerika
Vijana wa siku hizi, mbioni kuharibika.

6. Na tabia nyemelezi, zinazoletwa Afrika
Ushoga ndio ushenzi, kwetu linafahamika
Twatakiwa kuuenzi, hadi ndoa kufungika
Vijana wa siku hizi, mbioni kuharibika.
7. Tumeona viongozi, Ulaya na Amerika
Ndoa hizi za kishenzi, wasema zaheshimika
Tusishangae mavazi, kwao yakivurugika
Vijana wa siku hizi, mbioni kuharibika.
8. Mtu japo awe chizi, asili ya Afrika
mume na mume hawezo, ndoa zao kuridhika
Kwa mujibu wa malezi, kwa wahenga
yameta
Vijana wa siku hizi, mbioni kuharibika
9. Nimewawekea wazi, vituko vya Amerika
Wasiigwe kwa mavazi, tabia na kadhalika
Vijana wa siku hizi, mbioni kuharibika
Vijana wa siku hizi, mbioni kuharibika.
10. Angalieni wazazi, vijana walipofika
Wamevalia majinzi, viunoni yametoka
Makalio yako wazi, vijana wameridhika
Vijana wa siku hizi, mbioni kuharibika
11. Vijana wana mapenzi, na mila za Amerika
Hawafanyi upekuzi, tuwaeleze hakika
Warekebishe mavazi, na tabia kadhalika
Vijana wa siku hizi, mbioni kuharibika.
12. Mwenzenu siwalalizi, vijana wa hili rika
Wananitia simanzi, hatua waliyofika
Haya yafanyiwe kazi, tupate kusalimika.
Vijana wa siku hizi, mbioni kuharibika.
13. Magambilwa ni mtunzi, wa beti hizi hakika,
Ameyaweka makazi, Dar es Salaam
Chanika
Msicheze na malezi, kwaherini naondoka
Vijana na siku hizi, mbioni kuharibika.

9. MTU WA KWANZA NI MWALIMU

1. Nyote nina wasalimu, wake na waume pia
Kuna mambo ya muhimu, leo nawaelezea
Ingawa mwayafahamu, yafaa kukumbushia
Napendekeza mwalimu, aitwe
mheshimiwa
2. Ninalia na walimu, popote walipokuwa
Mwenzenu na waheshimu, siwezi kuelezea
Hawa ni watu muhimu, kila pembe ya dunia
Napendekeza mwalimu aitwe mheshimiwa
3. Kila anayefahamu, vitabu kujisomea
Kapitia kwa mwalimu, kila mtu aeleva
Wamepita kwa mwalimu, hata watunga
sheria
Napendekeza mwalimu, aitwe
mheshimiwa.
4. Ukiuona Hakimu, na Waziri washeria
Kawafundisha mwalimu, hadi walipofikia,
Marais na Makamu, na wabunge wote pia
Napendekeza mwalimu, aitwe
mheshimiwa.
5. Wahandisi wanajimu, na wasomi wote pia,
Ukila kitu kitamu, unachokifurahia
Kafundishwa na mwalimu, alokutengenezea
Napendekeza mwalimu, aitwe mheshimiwa.
6. Daktari ni muhimu, kila mtu aeleva
Aokowa mahakimu, na kila waheshimiwa
Kafkishwa na mwalimu, hapo alipofikia.
Napendekeza mwalimu, aitwe mheshimiwa.
7. Aliyegundua simu, na ndege zinazopaa
Kila nyanja ya Elimu, utakayofikiria
Mtu wa kwanza mwalimu, aliyemuweka
sawa
Napendekeza mwalimu, aitwe mheshimiwa.

MASHAIRI YA KIJAMII

8. Nalinganisha mwalimu, na kila muheshimiwa
Jinsi alivyo muhimu, katika kuhudumia
Nikamuona mwalimu, kawashinda wote pia
Napendekeza mwalimu, aitwe
muheshimiwa.
9. Nikagundua mwalimu, hodari kuvumilia
Yale maisha magumu, wengi tunayakimbia
Mlezi wetu mwalimu, yupo kwa kila mkoa
Napendekeza mwalimu, aitwe
muheshimiwa
10. Kabla sijafahamu, walimu wamekomaa
Nikadhania walimu, ni watu walozubaa
Kumbe ni wataalamu, wajua kuvumilia
Napendekeza mwalimu, aitwe
muheshimiwa
11. Ukimkuta mwalimu, kibanda anachokaa,
Kwake jambo la muhimu, elimu yake kutoa
Somo tukilifahamu, mwalimu afurahia
Napendekeza mwalimu, aitwe
muheshimiwa
12. Kwa niaba ya walimu, kila mtu namwambia
Amuheshimu mwalimu, ni mzazi wake pia
Mishahara ya walimu, ipandishwe mara mia
Napendekeza mwalimu, aitwe
muheshimiwa
13. Mungu kaleta walimu, walio tutangulia
Mzazi wetu Adamu, Elimu aliyopewa
Kufundisha wanadamu, Mola kamuagizia
Napendekeza mwalimu, aitwe
muheshimiwa
14. Mkitaka kufahamu, nani amewatungia
Ni mtoto wa Adamu, Juma bin Magambilwa
Mtumishi wa walimu, beti hii naishia
Napendekeza mwalimu, aitwe
Muheshimiwa.

10. SAYARI YA KIELIMU

1. Nyote ni ndugu wa damu, kila mara nakariri
Ndivyo ninavyofahamu, wengi wenu
mnakiri
Kila nikiwasalimu, naisikia fahari
Tuitafute elimu, ikibidi tusafiri
2. Ninatangazo muhimu, kulikosa ni hatari
Linahimiza elimu, ndizo funguo za heri
Mwenye kukosa elimu, ninampa tahadhari
Tuitafute elimu, ikibidi tusafiri
3. Sijui mnafahamu, wabunge na mawaziri
Mabalozi mahakimu, walifanya ujasiri
Kuitafuta elimu, leo inawastiri
Tuitafute elimu, ikibidi tusafiri
4. Kuna maisha magumu, huko mbele ya safari
Muuza nyanya na ndimu, awe na cheti
kizuri
Pia awe na elimu, hata muosha magari
Tuitafute elimu, ikibidi tusafiri
5. Mziba magurudumu, pancha za motokari
Naye bila ya elimu, atakosa muajiri
Muuza icecream, naye asome vizuri
Tuitafute elimu, ikibidi tusafiri
6. Kitendo bila elimu, maishani ni hatari
Usiikwepe kalamu, vitabu na daftari
Usafishe ufahamu, hisia na tafakuri
Tuitafute elimu, ikibidi tusafiri
7. Tumefikia awamu, katika hii sayari
Tupiganie elimu, kwa kasi nguvu na ari
Ni sawa na marehemu, asiyé kuwa tarayi
Tuitafute elimu, ikibidi tusafiri
8. Dhana kuu ya elimu, ni kutuweka vizuri
Tukitumia elimu, twafanya kazi vizuri
Watu wata tuheshimu, kuntuona majasiri
Tuitafute elimu, ikibidi tusafiri

MASHAIRI YA KIJAMII

9. Unapokosa elimu, japo ukiwa tajiri
Rahisi kukudhulumu, utakaye muajiri
Hilo sote twafahamu, halitaki tafsiri
Tuitafute elimu, ikibidi tusafiri.
10. Elimu iwe elimu, kutenda kwa uhodari
Haitokuwa elimu, nadharia kukariri
Ukijifunza elimu, kwa vitendo tafsiri
Tuitafute elimu, ikibidi tusafiri.
11. Mmoja wa Maimamu, kasoma kwa
Mukhtari
Milango ya kielimu, Elfu kaikariri
Kila lango la elimu, kalielewa vizuri
Tuitafute elimu, ikibidi tusafiri.
12. Asema yule Imamu, Elimu nimehariri
Kila lango la elimu, nimeleta utitiri
Milango ya ki-elimu, milioni imejiri
Tuitafute elimu, ikibidi tusafiri.
13. Ukipita kwa mwalimu, kujifunza mstari
Ikiwa umefahamu, nawe toa mstari
Huko ndiko kufahamu, ndugu zangu siyo
siri
Tuitafute elimu, ikibidi tusafiri.
14. Tuichukue elimu, ipate kutusitiri
Mkitaka kufahamu, nani katunga shairi
Naweka chini kalamu, Juma Saidi Nasri
Tuitafute elimu, ikibidi tusafiri.
3. Faida kubwa ya ndoa
Msingi wa familia
Familia bila ndoa
Ni vituko vya dunia.
4. Ndugu zao wanandoa
Wakaa wakielewa
Ndugu yao kaolewa
Ndugu mume ameowa.
5. Siku ya kufunga ndoa
Umma unashuhudia
Wawili wameamua
Kuanzisha familia
6. Watu wanashangilia
Kwa mume na mke pia
Mume mfalme kawa
Na mke ni malikia.
7. Mtoto akizaliwa
Pande zote zinajua
Kila mtu apupia
Jina lake kulitoa.
8. Wazazi wataamua
Namna ya kumlea
Mwana anavyolelewa
Ndivyo atakavyokuwa.
9. Ataziona huruma,
Toka kwa baba na mama
Atakuwa mtu mwema
Mkubwa akishakua
10. Mwana wa baba na mama
Hapa baba hapa mama
Hayo ni malezi mema
Mtoto ajivunie
11. Uzazi wenye lawama
Ni mimba za kwenye ngoma
Akijifunguwa mama
Baba aweza kataa

11. FUNGENI NDOA

1. Naanza kusalimia
Naomba kuitikiwa
Nipate kuwausia
Mambo yenze manufaa
2. Nawahimizeni ndoa
Ewe mwanamume oa
Mwana wa kike olewa
Mambo yataenda sawa.
10. Mwana wa baba na mama
Hapa baba hapa mama
Hayo ni malezi mema
Mtoto ajivunie
11. Uzazi wenye lawama
Ni mimba za kwenye ngoma
Akijifunguwa mama
Baba aweza kataa

MASHAIRI YA KIJAMII

12. Japo akirudi nyuma
Kuhudumia mama
Wadanganya watagoma
Mtoto kumtambua
13. Japo kuwa mahakama
Zitamtambua mama
Nakuamuru gharama
Mtoto kuhudumiwa
14. Raha ya baba na mama
Mtoto mmemnyima
Ni kama nusu yatima
Au mwana wa mtaa
6. Mimi naona ni vyema, kukusanya mataifa
Lakini mbona unyama, ukatili na maafa
Wanyonge wanalalamu, umoja wa mataifa
Tufanye tunayosema, umoja wa mataifa.
7. Matukio ya kinyama, baadhi ya mataifa
Wakimbizi wanahama, kiyaepuka maafa
Baraza linatazama, umoja wa mataifa
Tufanye tunayosema, umoja wa mataifa.
8. Baraza la usalama, umoja wa mataifa
Ubabe na uhasama, leo hii ndio sifa
Mnajali usalama, baadhi ya mataifa
Tufanye tunayosema, umoja wa mataifa
9. Ulimwengu unazama, maadili yamekufa
Binadamu na mnyama, wanafanana kwa sifa
Maneno mnayosema, na matendo ni masafa.
Tufanye tunayosema, umoja wa mataifa

12. TUFANYE TUNAYOSEMA

1. Nawatakia salama, watu wakila taifa
Tumuombeni Karima, atuepushe maafa
Atuongeze hekima, busara na maarifa
Tufanye tunayosema, umoja wa mataifa
2. Na sisi ni kama umma, hakuna mpenda kufa
Sasa tusimame wima, kwa mbinu na
maarifa
Tuepuke kulalama, na kuchafuana sifa
Tufanye tunayosema, umoja wa taifa
3. Tunaishi kwenye zama, zimejaa maarifa
Wenzetu siku za nyuma, walikosa taarifa
Leo tunayatazama, mambo ya kilaTaifa
Tufanye tunayosema, umoja wa mataifa.
4. Wenzetu wa huko nyuma, Libya watu
wakifa
Hawatojua mapema, na kupata taarifa
Sisi twajua mapema, na kushudia maafa
Tufanye tunayosema, umoja wa mataifa.
5. Hajatokea zama, kukusanya mataifa
Baraza la usalama, umoja wa mataifa
Ajibu ya hizi zama, tumepeata hii sifa
Tufanye tunayosema, umoja wa mataifa.
10. Kila nikiwatizama, umoja wa mataifa
Hamleti usalama, wa kweli kwa mataifa
Mnalinda usalama, baadhi ya mataifa
Tufanye tunayosema, umoja wa mataifa.
11. Palestina tazama, wanadamu wanakufa
Nyinyi mnachotazama, yahudi asijekufa
Mwingine mwamtazama, kama nyoka sasa
kafa
Tufanye tunayosema, umoja wa mataifa.
12. Sote ni watu wazima tumepewa maarifa
Kudanganyana lazima, kutomezwe na kufa
Kutenda unachosema, yapendeza hii sifa
Tufanye tunayosema umoja wa mataifa.
13. Beti hii nasimama, umoja wa mataifa
Kwa jina naitwa Juma, Tanzania utaifa
Naishi Darisalaama, chanika yangu tarafa
Tufanye tunayosema, umoja wa mataifa

13. KUHUSU MWENYEZI MUNGU

1. Hamjambo ndugu zangu, uzima na watakia
Mimi njema hali yangu, Mola anihudumia
Atosha Mwenyezi Mungu, muumba hii
dunia
Kuhusu Mwenyezi Mungu, jambo la
kufikiria.
2. Naja na maswali yangu, mnijibu sawa sawa
Wewe kiumbe wa Mungu, hivi unafikiria
Alivyo tumbu Mungu, nini kakikusudia
Kuhusu Mwenyezi Mungu, jambo
lakufikiria.
3. Ona aridhi na mbingu, Mola kaviweka sawa
Nyota mafungu mafungu, bahari mito
maziwa
Mimea ya ulimwengu, mvua mwezi na jua
Kuhusu Mwenyezi Mungu, jambo la
kufikiria.
4. Kama si Mwenyezi Mungu, tungepata wapi
hewa
Nafaka maji na dengu, matunda chai
kahawa
Vitunguu nyanya chungu, tangawizi na
bamia
Kuhusu Mwenyezi Mungu, jambo la
kufikiria
5. Katupa Mwenyezi Mungu, macho bila
kulipia
Jua la Mwenyezi Mungu, sote tunalitumia
Bili yake ndugu zangu, nani anayelipia
Kuhusu Mwenyezi Mungu, jambo la
kufikiria
6. Maji ya Mwenyezi Mungu, bure
tunayatumia
Hewa safi ndugu zangu, twavuta na
kupumua

Yote kayafanya Mungu, tupate kumtambua
Kuhusu Mwenyezi Mungu, jambo la
kufikiria

7. Baadhi ya ndugu zangu, mwazidi kujichetua
Mwasema hakuna Mungu, mkila
mkivimbiwa
Adhabu kali kwa Mungu, hawa ina
wangojea
Kuhusu Mwenyezi Mungu, jambo la
kufikiria
8. Nawaasa ndugu zangu, tuanze kufikiria
Ana lengo gani Mungu, kuyafanya yote
haya
Kwenye vitabu vya Mungu, lengo
limeelezwa
kuhusu Mwenyezi Mungu, jambo la
kufikiria
9. Hebu turudi kwa Mungu, shukurani kuzitoa
Muumba nchi na mbingu, apate kuturudia
Huo ndiyo uchamungu, lengo tulilo umbiwa
Kuhusu Mwenyezi Mungu, jambo la
kufikiria
10. Mwisho wa shairi langu beti hii naishia
Juma ndio jina langu Daressalaam nakaa
Chanika nyumbani kwangu, ilala manipaa
Kuhusu Mwenyezi Mungu, jambo la
kufikiria.

14. MADHUMUNI YA HUSUDA

1. Salamu kaka na dada, na wadogo zangu pia
Nimewaletea mada, yatuhusu sote pia
Yaelezea husuda, na madhara yake pia
Kwa kila mwenye husuda, moyoni anaugua.
2. Hili gonjwa la husuda, wengi limeshawaua
Hata wafanya ibada, wengi wanaugulia
Leo natoa msaada, jinsi ya kujinasua
Kwa kila mwenye husuda, moyoni anaugua.

MASHAIRI YA KIJAMII

3. Maana yake husuda, mgonjwa afurahia
Maisha yanapododa, wenzake wakiumia
Wakipewa misaada, rohoni anaugua
Kwa kila mwenye husuda, moyoni anaugua.
4. Watu wakipata shida, hasidi ashangilia
Wakitoka kwenye shida, vibaya ajisikia
Wakipata cha ziada, hasidi augulia
Kwa kila mwenye husuda, moyoni anaugua.
5. Biashara zikidoda, mitaji ikififia
Tabasamu la ziada, hasidi atalitoa
Wakijapata faida, hasidi anyong'onyea
Kwa kila mwenye husuda, moyoni anaugua.
6. Ushauri wa ziada, hasidi nampatia,
Kuzichukia faida, sawa na kujichukia
Mungu hutoa ziada, analolitaka huwa
Kwa kila mwenye husuda, moyoni anaugua.
7. Kwa mtu mwenye husuda, aweza kusafiria
Unguja hadi Singida, lengo kukuharibia
Ukivaa midabwada, aona kafanikiwa
Kwa kila mwenye husuda, moyoni anaugua
8. Gonjwa hili la husuda, limetusababishia
Wasomi wenyе shahada, uongozi kuzuiwa
Watatumiwa makada, majina kuwachafua
Kwa kila mwenye husuda, moyoni anaugua.
9. Watapangwa na mabudha, kukuhubiri
vibaya,
Na watu wenyе sijida, mambo watakuzushia
Waseme una vimada, kila kona ya mtaa
Kwa kila mwenye husuda, moyoni anaugua.
10. Roho ya mwenye husuda, Wallahi inaugua
Anapowacha husuda, roho yaweza tulia
Na kurudi kwenye ada, kama alivyozaliwa
Kwa kila mwenye husuda, moyoni anaugua.
11. Upande wa kina dada, mwenzao akiolewa
Akijimudu kwa muda, visa watamfanyia
Hadi akakae Eda, kaachwa ama kafiwa
12. Kwa kila mwenye husuda, moyoni anaugua.
Kwa hapa sina ziada, beti hii naishia
Jina msipate shida, Juma mwana
Magambilwa
Naikataza husuda, tupate kufanikiwa
Kwa kila mwenye husuda, moyoni anaugua.

15. UTAMU WA KUSENGENYA

1. Rwanda Burundi na Kenya, Uganda na
Tanzania
Nimekuja kuwakanya, Kiswahili mwaelewa
Mpate kuyatawanya, katika yote dunia
Utamu wa kusengenya, unalizamisha juu.
2. Maradhi ya kusengenya, yaitafuna dunia
Virusi vyake vyapenya, kwenye roho
vinakaa
Mgonjwa anajifanya, kila kitu akijua
Utamu wa kusengenya, unalizamisha juu.
3. Maana ya kusengenya, ni kumzungumzia
Mtu bila kumuonya, awache mambo
mabaya
Maneno kuyatawanya, kisogo akishatoa
Utamu wa kusengenya, unalizamisha juu.
4. Mtu anayesengenya, ni yule aloishiwa
Na kutaka kujifanya, wenzake wanakosea
Wakiondoka husonya, na kuanza kukosoa
Utamu wa kusengenya, unalizamisha juu.
5. Vinara wa kusengenya, vijiweni wakikaa
Wakikosa la kufanya, watu huwaongelea
Macho yao huyabinya, kwa kila mpita njia
Utamu wa kusengenya, unalizamisha juu.
6. Wengine wanajifanya, wajimudu sawa sawa
Mtu akiuza nyanya, humsema kaishiwa
Wengine wanadanganya, kwao mabilionea
Utamu wa kusengenya, unalizamisha juu.

7. Kina mama hujifanya, matembele kuchambua
Nakukata bilinganya, kwa vikundi wanakaa
Lengo lao kusengenya, watakaye mchagua
Utamu wa kusengenya, unalizamisha jua.
8. Magwiji wa kusengenya, muembeni watakaa
Ukindu watautoa, mikeka kujishonea
Ni kutwa watasengenya, hadi kuzama kwa jua
Utamu wa kusengenya, unalizamisha jua.
9. Ulevi wa kusengenya, kwa uliyemkolea
Aweza kutoka Kenya, kuja hapa Tanzania
Habari kuzikusanya, gharama ataitoa
Utamu wa kusengenya, unalizamisha jua.
10. Wengineo hujifanya, wageni kuwapokea
Wapate kuwadanganya, fulani mtu mbaya
Tafadhali nakuonya, usije kumzowea
Utamu wa kusengenya, unalizamisha jua.
11. Madhara ya kusengenya, mtu anayekukosea
Makosa atayafanya, kwa kurudia rudia
Iwapo ungemuonya, aweze kujikosoa
Utamu wa kusengenya, unalizamisha jua.
12. Nguvu unazotawanya, katika matendo haya
La maana ungefanya, hadi ukajikwamua
Madhali umesengenya, fursa imepotea
Utamu wa kusengenya, unalizamisha jua.
13. Watu wanaosengenya, ni wengi kupinduka
Wale wasiosengenya, ni mmoja kila mia
Tukiwacha kusengenya, twaweza kufanikiwa
Utamu wa kusengenya, unalizamisha jua.
14. Beti nilizokusanya, ya mwisho namalizia
Juma ndiyе kawaonya, mtoto wa Magambilwa
Dawa yaweza kuponya, gonjwa likatokomea
Utamu wa kusengenya, unalizamisha jua.

16. KIBURI SIMAUNGWANA

1. Nina watakia kheri, ndugu zangu waungwana
Najisikia vizuri, kila tunapokutana Kupeana ushauri, kwaleta faida sana
Wahenga wamekariri, kiburi si maungwana.
2. Leo naja na habari, muizingatie sana Majivuno na kiburi, umma vinautafuna Vimevuka mstari, watu wanabaguana Wahenga wamekariri, kiburi si maungwana.
3. Gonjwa la kisirisiri, vigumu kujulikana Hasa watu mashururi, wanajisahau sana Wathamini matajiri, kwao ndio wamaana Wahenga wamekariri, kiburi si maunguwana
4. Ulimwengu unakiri, watu wanabaguana Kwa rangi na utajiri, kila mtu anaona Hili siyo jambo zuri, halipendi Subhana Wahenga wamekariri, kiburi si maungwana
5. Niipi rangi nzuri, ipi rangi mbaya sana Hadi tufanye jeuri, na kudharauliana Tuelezane vizuri, haifai kufichana Wahenga wamekariri, kiburi si maungwana.
6. Niipi raangi nzuri, wapi inapatikana Tutoke alfajiri, tukainunue sana Kama si hivyo jeuri, wapi inapatikana Wahenga wamekariri, kiburi si maungwana
7. (Ubaguzi Mashauri, wa rangi tumeshaona Kwa wenye nia nzuri, watauepuka sana Rangi zote ni nzuri, kazileta Subhana Wahenga wamekariri, kiburi si muangwana
8. Ubaguzi wa kisiri, wengine hawaajaona Wasomi na matajiri, kwa ubora wajiona Majivuno na kiburi, msomi kazidi sana Wahenga wamekariri, kiburi si maungwana.

MASHAIRI YA KIJAMII

9. Wasomi wanafikiri, wao maalimu sana
Uwezo wakufikiri, watu wengine hawana
Hata akili nzuri, wengine wote hawana
Wahenga wamekariri, kiburi si maungwana
10. Kimejificha kiburi, kwenye giza nene sana
Kama mwana utitiri, na jiwe jeusi sana
Japo yumo utitiri, vigumu kuonekana
Wahenga wamekariri, kiburi si muangwana
11. Masheikh watahubiri, kiburi kuepukana
Wengi hawana habari, wenyewe
kimewabana
Kusema ni mahodari, kutenda yashindikana
Wahenga wamekariri, kiburi si maungwana
12. Wasomi na matajiri, ni mabibi na mabwana
Nyinyi watu mashuhuri, mnaheshimiwa
sana
Elimu kama bahari, na hivyo mwisho haina
Wahenga wamekariri, kiburi si maungwana
13. Hadhi na cheo kizuri, visingelipatikana
Umma ukiwa jeuri, kisha kukubaliana
Wasomi ni kama ngiri, kuwahishimu hakuna
Wahenga wamekariri, kiburi si maugwana
14. Mwisho halali shairi, kituo ni hiki bwana
Juma Saidi Nasiri, Magambilwa amanena
Muyachukue vizuri, kwa vitendo
waungwana
Wahenga wamekariri, kiburi si maugwana.
3. Kukemea utapeli
Jinsi ulivyoenea
4. Kupotoka maadili
Lafanana jambo hili
Gari lizame mtoni
Na huku linatembea
5. Maisha ya utapeli
Kwenye kada mbali mbali
Huu ndiyo muhimili,
Wanaoutegemea
6. Wageni wamepata mali
kwa njia ya utapeli
wakanenepesha miili
roho zimejeruhiwa.
7. Usisikie halali
Likitajwa neno hili
Lanaki kwenye kauli
Rohoni limepotea
8. Mataifa toka mbali
Dunia yaitapeli
Nakuujizolea mbali
Wanyonge wateketea
9. Ulafi na utapeli
Umefikia mahali
Ulimwengu umefeli
Kupitia mambo haya
10. Wahanga wa utapeli
Wateseka kweli kweli
Mataifa mbali mbali
Raia wanakimbia

17. UTAPELI

1. Ninawauliza hali
Wa karibu na mbali
Watu wa kila mahali
Katika hii dunia
2. Katika jukwaa hili
Nimeingia kamili
9. Wahanga wa utapeli
Wateseka kweli kweli
Mataifa mbali mbali
Raia wanakimbia
10. Masikini hawalali
Wakitafuta ugali
Matajiri hawalali
Wasije kutapeliwa

MASHAIRI YA KIJAMII

11. Wakubwa wa nchi mbili
Ukiwakuta pahali
Mmoja wao tapeli
Mwenzake amvizia
12. Ampore zake mali
Kwa mikataba batili
Ni kumchota akili
Huku akimchekea
13. Haufai utapeli
Wapingana na akili
Heshima na maadili
Dunia vyaiokoa
14. Haufai utapeli
Tudumishe maadili
Leo sintoenda mbali,
Beti hii meishia.
5. Alama za mnafiki
Sita hazibadlik
Mimi nimezihakiki
Sikia nakutajia.
6. Akisema mnafiki
Muongo hasemi haki
Na kamwe haaminiki
Kwa ahadi akitoa
7. Sura yake mnafiki
Yavutia kama keki
Rohoni hakusomeki
Anajisikia kuwa.
8. Maneno ya mnafiki
Yananukia iliki,
Matendo akishiriki
Analegealegea
9. Umbo lake mnafiki
Linanukia miski
Roho haikubaliki
Yatoa harufu mbaya

18. KIWANDA CHA UNAFIKI

1. Hamjambo halaki
Jirani na mnafiki
Mola akitubariki
Kidogo nitaongea
2. Kiwanda cha unafiki
Mwenzenu siafiki
Bali hakikubaliki
Kwa kila anayejua
3. Rangi yake unafiki
Huja kama urafiki
Roho imejaa chuki
Imefichwa sawa sawa
4. Maradhi ya unafiki
Yasumbua halaiki
Magharibi Mashariki
Wagonjwa wameshajaa.
10. Ateseka mnafiki
Kwa kuichukia haki
Ni sawa na boyo haki
Baharini yaelea
11. Boya halifunikiki
Kujificha halitaki
Hata ufanye mikiki
Lazima litaelea
12. Kilio cha mnafiki
Ni kuifunika haki
Kwa vishindo na mikiki
Haki bado yaelea.
13. Atakalo mnafiki
Abaki hafahamiki
Apate kustahiki
Pande zote kuingia

MASHAIRI YA KIJAMII

14. Kituo changu ni hiki
Nataisha kisa hiki
mtunzi wenu rafiki
Juma mwana Magambilwa.

19. KISIRANI

1. Ndugu zangu hali gani
Watu wote duniani
Wa mbali na majirani
Salamu nawatolea
2. Nimerudi jukwaani
Kuna nilichobaini
Watu wenyе kisirani
Wateseka na dunia.
3. Ugonjwa wa kisirani
Hupita ndani kwa ndani
Na kufunika kiini
Cha akili kupotea
4. Kamtazame usoni
Mtu mwenye kisirani
Ni majuto na huzuni
Vilivyomuelemea
5. Akiwa kwenye foleni
Kuelekea kazini
Jasho jembamba usoni
Mwake limetapakaa
6. Barabara atamani
Ipitishwe hewani
Kuliko ile foleni
Inayomuelemea
7. Kwenye taa za kijani
Zilizo barbarani
Zamuumiza moyoni
Kupisha wapita njia
8. Akiingia kazini
Aenda kwanza chooni

- Akiikuta foleni
Anaweza kuzimia
9. Akitoka msalani
Nakupenda kantini
Nako akute foleni
Wenzake huwachukia

10. Mtu mwenye kisirani
Ni mgonjwa taabani
Kila kitu duniani
Kwake ni kitu kibaya

11. Nami natoa maoni
Kuondoa kisirani
Ni kukubali moyoni
Kuchukia siyo dawa

12. Vile vile tuamini
Machafuko ya rohoni
Yanaleta kisirani
Ndipo tunajichukia.

13. Usitafute thamani
Kwa watu wa duniani
Mola atakuthamini
Njia ukiipatia

14. Nawaaga kwaherini
Naenda kukaa chini
Aliye kutungieni
Juma mwana Magambilwa

20. HOFU

1. Ndugu zangu watukufu
Leo nawataarifu
Nimegundua hofu
Inavyotuharibia
2. Tunapoitaja hofu
Jina hili maarufu
Ila hakika ya hofu
Wengi hawajaijua

MASHAIRI YA KIJAMII

3. Uhakika wake hofu
Jina hili maarufu
Inaiongoza safu
Ya walionyong'onyea
4. Mtu akiwa na hofu
Mwili huwa kama gofu
Viungo kama mkufu
Vinalegea legea
5. Moyo ulio na hofu
Daima huwa dhaifu
Kukosa ubainifu
Lipi zuri lipi baya
6. Tatizo la mwenye hofu
Ile ya muda mrefu
Huwa yamtaarifu
Kushindwa na kulegea
7. Haoni ukamilfu
Anahisi mapungufu
Anajihesabu mfu
Hana wa kumuokoa
8. Dawa ya kushinda hofu
Ni kujuwa nini hofu
Rangi gani na harufu
Inayobainikia
9. Nini hiki hofu
Kwa nini uwe na hofu
Hofu ya muda mrefu
Waweza pata kichaa
10. Ziandike kila hofu
Halafu uzisanifu
Ziambie wewe hofu
Wacha kuniongopea
11. Moyo ukiwa mchafu
Ni kimbillio la hofu
Husababisha mapafu
Yasimudu kupumua
12. Huo ndio uzoefu
Kuhusu mdudu hofu
Husababisha mapafu
Yasimudu kupumua
13. Jipange bila ya hofu
Utapata marudufu
Huu ndiyo uzoefu
Niliokukusanya.
14. Mazumgumzo marefu
Wengine yatawakifu
Kwaherini watukufu
Mimi Juma Magambilwa

21. VUNO LA MTU MUOGA

1. Kengele ninaipiga
Wasikie wa Msoga
Kasulu hadi Kwachaga
Vijiji vyta Tanzania
2. Hofu tumeshaiiga
Tumebaki na uoga
Kitu hofu na uoga
Vyafanana kwa tabia
3. Mtu akiwa muoga
Mipango huivuruga
Hata kuku wa kufuga
Hawezi kumchukua
4. Akipita kwenye mbuga
Akakutana na Twiga
Yeye atachanja mbuga
Nakuanza kukimbia.
5. Akimkuta kinega
Mayai ameyataga
Ataogopa kinega
Asije kumparura.
6. Chura akimkanyaga
Ama akiguswa bega

MASHAIRI YA KIJAMII

- Mwingi aloaja woga
Aweza akakimbia.
7. Buibui akitega
Uzi wake akimwaga
Ukimgusa muoga
Ukelele atatoa.
8. Akiuona mzoga
Mtu aliye na woga
Adhani chui katega
Hivyo kubadili njia
9. Mtu akiwa muoga
Aweza kukosa mboga
Hata bata wa kufuga
Kumchinja ahofia.
10. Mashine zinaposaga
Makelele zikipiga
Masikio ya muoga
Yanahisi kuvamiwa.
11. Kiumbe wacha uoga
Unga wako utamwaga
Chumvi viungo na mboga
Watoto wafe na njaa.
12. Kwa kila mtu muoga
Kazi zake huvuruga
Kuhama bila kuaga
Mara nyingi hutokea
13. Matatizo ya uoga
Nasema kinaganaga
Hakuna kinachonoga
Bila ya kikitibua
14. Maongezi yamenoga
Na dakika zimeaga
Beti hii nawaaga
Mtunzi ni Magambilwa.

22. WIZI NA UJAMBAZI

1. Habari za saa hizi
Wakongwe na chipukizi
Nakuja na simulizi
Zaweza tusaidia.
2. Leo na kemea wizi
Kwa ukweli na uwazi
Kujizuia siwezi
Jambo hili kukemea.
3. Adui mwingine mwizi
Hapendi kufanya kazi
Wala kulima viazi
Kazi yake kuvizia
4. Wala kuuza mavazi
Ukimshauri mwizi
Ima kazi ya Ulinzi
Lazima atakataa.
5. Hata kuuza dalanzi
Na makuti ya minazi
Japo kuuza masinzi
Mwizi atayakataa
6. Mwizi gaba usingizi
Akesha kwenye mvizi
Na kufanya uvamizi
Walinzi wakisinzia
7. Mtu huyu hapendezi
Amekosa mtetezi
Hata baba na shangazi
Mwizi wanamchukia.
8. Ndugu yangu wacha wizi
Jifunze kufanya kazi
Nakuonya kwa mapenzi
Upate kuokolewa
9. Raia wa siku hizi
Kusubiri hawawezi

MASHAIRI YA KIJAMII

- Wakimkamata mwizi
Moto wanamlipua
10. Ukishakomaa wizi
Hugeuka ujambazi
Ukifika hii ngazi
Umeshapotea njia
11. Kawaida ya jambazi
Akifanya hiyo kazi
Baba mama na shangazi
Hatoshindwa kuwaua.
12. Kama mwanao jambazi
Muonye ewe mzazi
Usijetoa machozi
Akiuliza vibaya.
13. Ndugu zangu majambazi
Wacheni hiyo si kazi
Muogopeni Mwenyezi
Muumba hii dunia.
14. Zinatosha beti hizi
Mkazifanyie kazi
Kutunza huu utenzi
Juma mwana Magambilwa
4. Ya kwamba mwenye Hiyana
Utulivu kwake hana
Mali zako akiona
Atamani kuchukua.
5. Hata mkielewana
Na mtu mwenye hiyana
Faida mtagawana
Haiwezi kutimia.
6. Yanisikitisha sana
Mtu kukupa amana
Kakuona wa maana
Wamkatisha tamaa.
7. Kwa mtu mwenye hiyana
Akiachiwa hazina
Wallahi mtamuona
Atakavyo wafanya.
8. Ni ugonjwa wa hiyana
Moyoni unatafunu
Si rahisi kuuona
Jinsi unavyoingia
9. Asili yake hiyana
Na husuda vyafanana
Moyoni vikikutana
Moyo unateketea

23. HIYANA

1. Kwa mabibi na mabwana
Hamjambo ninaona
Mimi ni mzima sana
Vyema ninajisikia.
2. Kuna kitu nimeona
Wengi hawajakiona
Jina lake ni Hiyana
Sijui mwaitambua
3. Ukisikia Hiyana
Ni kukiuka Amana
Ukiwekewa Amana
Wewe ukaitumia.
10. Ili kuacha hiyana
Mbona ni rahisi sana
Jitahidi kuwaona
Watu wakifanikiwa.
11. Wenye shida ukiona
Waponye haraka sana
Kwako jambo la maana
Watu wakifanikiwa
12. Usihitaji ubwana
Nakuwaona watwana
Ukiwekewa Amana
Hakikisha zarejea.

MASHAIRI YA KIJAMII

- | | |
|---|---|
| 13. Jizoweshe kupeana
Kisha kurejesheana
Hadi hapo utaponia
Hiyana itakimbia. | Au awe sisiminzi
Kuliko mateso haya |
| 14. Kwa heri ya kuonana
Ipige vita hiyana
Mtnzi wenu ni bwana
Juma mwana Magambilwa. | 8. Bahati mbaya uzinzi
Kwa watu wa siku hizi
Wafanyika wazi wazi
Watoto washuhudia |
| | 9. Watoto wa siku hizi
Wajifundisha uzinzi
Kwa kuwaona wazazi
Pombe zikiwakolea. |

24. SHIMO LA HATARI

- | | |
|---|--|
| 1. Kabla ya maongezi
Yetu ya huu Utensi
Nachukua maamuzi
Kwanza huwasalimia. | 10. luniga nasema wazi
Zinachochea uzinzi
Kisa ni utandawazi
Wanao usingizia |
| 2. Nakuja kufanya kazi
Kuukemea uzinzi
Zama za utadawazi
Zina imetapakaa | 11. Kiumbe wacha uzinzi
Amekekataza Mwenyezi
Bora katafute mwenzi
Mpate kufunga ndoa. |
| 3. Kwa bahati yako wazi
Kwa wazima na machizzi
Matookeo ya uzinzi
Wote wanayaelewa | 12. Zinaa haipendezi
Kaikataza Mwenyezi
Hata mila za kishenzi
Zaikataza zinaa |
| 4. Mtu akiwa mzinzi
Yuko kwenye utelezi
Wa kifo cha waziwazi
Nakuihama dunia | 13. Madhara ya wazi wazi
Hata bila upekuzi
Yamngoeja mzinzi
Ili aje kuyavaa |
| 5. Magonjwa yaliyo wazi
Hayasikii mzizi
Yamvizia mzizi
Hatimaye kumuua | 14. Zinatosha beti hizi
Za ukweli na uwazi
Aliyetunga utenzi
Juma mwana Magambilwa |
| 6. Ukimwi na fumanizi
Na mimba kwa wanafunzi
Ndiyo shimo la mzinzi
Atakalotumbukia | |
| 7. Atalalama mzinzi
Bora angeumbwa inzi | |

25. UONGO

1. Hodi nagonga mlango, kila nyumba naingia
Huku nimeshika bango, linalotuelezea

MASHAIRI YA KIJAMII

- Utapeli na uongo, vyaitafuna dunia
Utapeli na uongo, hizo ni tabia mbaya.
2. Kuzungumza uongo, wengi wanakimbilia
Ikibidi hata hongo, kutoa na kupokea
Utapeli na uongo, hizo ni tabia mbaya
3. Umepasishwa uongo, miji yote ya dunia
Daresalamu ni bongo, jina tulilozoea
Kwa kughushi na uongo, riziki kujipatia
Utapeli na uongo, hizo ni tabia mbaya.
4. Ukiingia Ubungo, kwenye gari za mikoa
Utayaona mabango, yanayokutangazia
Kila moja lina lengo, kutaka kukuvutia
Utapeli na uongo, hizo ni tabia mbaya.
5. Ni kituo cha Ubungo, kabla hujaingia
Mawakala wa uongo, furushi hukupokea
Na tiketi za uongo, aweza kukuuzia
Utapeli na uongo hizo ni tabia mbaya.
6. Dar es Salaam ni bongo, jina tulilozoea
Hata muuza matango, uongo atumia
Asema haya matango, Ulaya yanatokea
Utapeli na uongo hizo ni tabia mbaya.
7. Dar es Salaam ni bongo, vitongoji na mitaa
Watu wanakunywa gongo, na unga
wanaubugia
Hulala kwenye majengo, yaliyojiangukia
Utapeli na uongo hizo ni tabia mbaya.
8. Dar es Salaam ni bongo, ukifika angalia
Hasa mtaa wa Kongo, unaweza kuibwa
Waweza kutiwa chongo, kama hawakukuua
Utapeli na uongo hizo ni tabia mbaya
9. Wale waganga waongo, mji huu wamejaa
Wanavyuoni waongo, Bongo wamekimbia
Na wachungaji waongo, Jiji hili wamejaa
Utapeli na uongo hizo ni tabia mbaya.
10. Waganga wana mabango, kila kitu watibia
Watahitaji viungo, vya mama alokuzaa
- Kukamilisha mipango, ukawe bilionea
Utapeli na uongo hizo ni tabia mbaya.
11. Wengine wana mabango, Mtume
yamzushia
Tiba zao za uongo, eti Sunna za Nabiya
Dhamira yao na lengo, watu wote kununua.
Utapeli na uongo, hizo ni tabia mbaya
12. Kwenye mitaa ya Bongo, ndugu unapoingia
Walemavu wa uongo, wataka kuhurumiwa
Na wewe chemsha bongo, usije
kudhulumiwa
Utapeli na uongo, hizo ni tabia mbaya
13. Kwenu natoa mchango, matapeli mwasikia
Uzeni hata mabungo, halali kujichumia
Jiwekeeni malengo, mpate kuheshimiwa
Utapeli na uongo hizo ni tabia mbaya
14. Nimefikia ukingo, beti hii naishia
Nasaha si masimango, ni kuonyeshana njia
Shairi hili ni tungo, za Juma wa
Magambilwa
Utapeli na uongo, hizo ni tabia mbaya.

26. UPENDO KIVITENDO

1. Waliopo na wa kando
Salaa ndiyo mwenendo
Ndiyo chanzo cha upendo
Tunaouhitajia.
2. Nimekuja na mafundo
Ya ufundisha upendo
Njooni mliyoko kando
Darasani naingia.
3. Tunaposema upendo
Dharau tuweke kando
Kisirani na mifundo
Popote tunapokuwa.

MASHAIRI YA KIJAMII

4. Watiririka upendo
Kama maji ya mkondo
Mbweha Nyani na Tolondo
Wanywa na kuogelea.
5. Unanukia upendo
Kwa hapa na kando kando
Manukato ya upendo
Yanuswa na kila pua.
6. Ladha ya mwenye upendo
Ni kueneza uhondo
Viumbe kila mtindo
Wote watahudumiwa.
7. Ukelele wa upendo
Mwanga hewa na kishindo
Rafiki na mwenye fundo
Wote utawafikia.
8. Uhakika wa upendo
Ni maneno na vitendo
Viwe katika mtindo
Uendao sawa sawa
9. Kinyume chake upendo
Watangazwa kwa kishindo
Masharti ya upendo
Ubaguzi hutumiwa.
10. Madalali wa upendo
Wao hawana vitendo
Wamepoteza mkondo
Kelele zimebakia.
11. Ukisikia upendo
Kwa dalali wa upendo
Yuko katika mawindo
Sadaka azivizia
12. Dalali kwake upendo
Biashara ya magendo
Ili apate marundo
Na kuwa milionea.
13. Tunahitaji upendo
Kwa maneno na vitendo
Ili wapate uhondo
Ndugu na adui pia
14. Nishati yake upendo
Yabadilisha mwenendo
Adui mwenye mifundo
Akabadili tabia.
15. Tujifunzeni upendo
Kama ndege Hondohondo
Roho ngumu kama Nyundo
Haitatusaidia
16. Wacha mawazo mgando
Ushike haya mafundo
Kalamu naweka kando
Beti hii naishia.

27. MIZOZO YA NINI

1. Salaam jambo la mwanzo
Haya kwetu ni mafunzo
Kabla ya vidokezo
Nyote nawasalimia.
2. Naleta mazungumzo
Muhimu na siyo gumzo
Kuhusu hii mizozo
Inayotuelemea.
3. Nashangazwa na mizozo
Kwenye vyuo vya mafunzo
Hadi timu za michezo
Mizozo yawasumbua.
4. Tunaelewa michezo
Tuseme nikiliwazo
Chakutuliza mawazo
Na mwili kuweka sawa.
5. Inakuwaje michezo
Ikawa si kiliwazo

MASHAIRI YA KIJAMII

- | | |
|--|--|
| Chakutuliza mawazo
Vurugu likaingiya. | Tuiepuke mizozo
Anasema Magambilwa. |
| 6. Tulitatue tatizo
Linaloleta mizozo
Tukijua tangu mwanzo
Tupate kulitatua. | |
| 7. Vyuo vikuu mizozo
Hospitali mizozo
Makazini ni mizozo.
Yaanzaje kuingia. | |
| 8. Tumeshangaa mizozo
Kwenye timu za michezo
Vyuo vikuu mizozo
Nazidi kuishangaa. | |
| 9. Elimu walizonazo
Hata shahada wanazo
Za kuhitimu mafunzo
Hadi diplomasia. | |
| 10. Elimu kubwa wanazo
Wamepanuka mawazo
Wako katika mafunzo
Wengine wanasheria. | |
| 11. Inapokuja mizozo
Mimi Napata mawazo
Wako katika mafunzo
Wengine wanasheria. | |
| 12. Tofauti ya mawazo
Hatukwepi kuwa nazo
Tuvikubali vigezo
Wengine wanapotoa. | |
| 13. Vikithibiti vigezo
Vipangue kwa vigezo
Wala siyo maelezo
Jina kumchafulia | |
| 14. Mwisho wanazungumza
Ninatilia mkazo | |

28. USILALAMIKE JIPANGE

1. Vipi mna hali njema
Mimi hali yangu njema
Ndiyo mana nasimama
Habari kuwaletea
2. Kuusiana lawama
Hii si tabia njema
Tuambiane mapema
Kabla ya kuzowea
3. Mwingine ana lawama
Ndugu kuwapa lawama
Asema wana mnyima
Jinsi ya kuendelea
4. Kukaa na kulalama
Na kazi zina simama
Azidi kubaki nyuma
Wenzake waendelea.
5. Maradhi ya kulalama
Hayaleti mwisho mwema
Hakuna anachochuma
Nduguze kuwachukia
6. Binadamu kama umma
Ametuumba Karima
Hatuna pakuegama
Ila kwa Mola Jalia
7. Ndugu ukimuegama
Uhuru una mnyima
Atakuchoka mapema
Ukija akukimbilia.
8. Wewe kama ni kilema
Madamu unalalama
Akili yako nzima
Waweza kuitumia

MASHAIRI YA KIJAMII

9. Kuna kazi za vilema
Baada ya kuzisoma
wangapi wanajituma
dhiki kujiandolea
10. Kusaidia vilema
Ni jambo lenye heshima
Wito kwa kila kilema
Ajjipange sawasawa
11. Mwenyezi Mungu ni mwema
Anawaona vilema
Ridhiki hatowanyima
Wallahi nawaapia
12. Na wengine ni wazima
Kutwa kucha walalama
Mtu wa hivi lazima
Nduguze kumkimbia
13. Wallahi tukijituma
Twapata natija njema
Nakuipata heshima
Tunayoihitajia
14. Beti hii nasimama
Shikeni niliyosema
Mimi naitwa Juma
utenzi nimeutoa.
4. Wasafiri wakikwama
Maskini na yatima
Mafukara na vilema
Mtu mwema huwafaa
5. Mungu Mwingi wa hekima
Kawapa baba na mama
Mapenzi hata huruma
Baada ya kutuzaa
6. Kwa mapenzi na huruma
Wazazi baba na mama
Wametumia gharama
Hadi twajitegemea
7. Tumelishwa tumesoma
Kwa wapenzi na huruma
Bila kujali gharama
Mwanadamu zingatia
8. Umefanyiwa huruma
Ili uwe mtu mwema
Ambaye utasimama
Viumbe kuwaokoa
9. Binadamu na wanyama
Wanahitaji huruma
Kutoka kwa mtu mwema
Ni wewe muheshimiwa
10. Sote tuwe na huruma
Kwa wajane na yatima
Vikongwe hata vilema
Na kila alozidiwa
11. Ndipo dunia nzima
Iwe ni sayari njema
Kwani haina hujuma
Vituko na roho mbaya
12. Beti hii nasimama
Nawatakia salama

29. HURUMA NI UTUWEMA

1. Jamani mko salama
Mimi afya yangu njema
Kuna jambo lakusema
Mambo kuyaweka sawa
2. Naihimiza huruma
Wababa na kina mama
Wengi wameshaihama
Yabaki historia
3. Kwa mtu mwenye huruma
Kwa watu hufanya wema
10. Sote tuwe na huruma
Kwa wajane na yatima
Vikongwe hata vilema
Na kila alozidiwa
11. Ndipo dunia nzima
Iwe ni sayari njema
Kwani haina hujuma
Vituko na roho mbaya
12. Beti hii nasimama
Nawatakia salama

MASHAIRI YA KIJAMII

Mtunzi aitwa Juma
Said wa Magambilwa.

9. Kuchukua maamuzi
Kwataka upambanuzi
Kuliooka jahazi
Lisije kudidimia

30. UTAWEZA UONGOZI

1. Habari kwa viongozi
Walimu na wanafunzi
Ndugu zangu na wazazi
Kwanza nawasalimia
2. Nimeamka kikazi
Nikiwa na maamuzi
Kuwaita viongozi
Nipate kuwausia
3. Ukiwa ni kiongozi
Wacha kazi fanyakazi
Wewe ni msimamizi
Ambarae wategemewa
4. Kiongozi ni mlinzi
Asiwe na usingizi
Akipanga utatuzi
Migogoro ya raia
5. Vile vile kiongozi
Hakika ndiye mlezi
Sawa na baba mzazi
Wote wamtegemea
6. Ahakikishe malazi
Chakula na matumizi
Masomo hata makazi
Hayasumbui Raia
7. Abuni usimamizi
Mzuri kuchapa kazi
Kuwapanga viongozi
Wakweli kisawasawa
8. Hakika ya uongozi
Akipewa mtambuzi
Atasema siuwezi
Kheri nibaki raia

9. Kuchukua maamuzi
Kwataka upambanuzi
Kuliooka jahazi
Lisije kudidimia
10. ukila nyama ya mbuzi
Ndizi na wali wa nazi
Watasema kiongozi
Hazina aitumia
11. Ukisafiri kikazi
Au kuona wazazi
Kwa Suzuki ama benzi
Macho utakodolewa
12. Kila siku ya Mwenyezi
Asengenywa kiongozi
Na kupangwa mapinduzi
Na baadhi ya Raia
13. Kwa ukweli na uwazi
Mbora wa viongozi
Aishi kwa matumizi
Sawa sawa na raia
14. Nafupisha beti hizi
Shikeni nasaha hizi
Juma Saidi Mtunzi
Nasoro wa Magambilwa.

31. UKIHAMAKI

1. Hamjambo marafiki
Magharibi mashariki
Hata mtu asibaki
Salaam nawatolea
2. Kusema kweli sichoki
Japo sio mshabiki
Wa kuona halaiki
Macho yanikodolea
3. Ila nikiona dhiki
Watu ikiwadiriki

MASHAIRI YA KIJAMII

- | | |
|---|--|
| Nafanya kile na hiki
Wenzangu kuwakomboa | Kataa kwa mantiki
Watu watakuelewa |
| 4. Kisa cha leo ni hiki
Kuna gonjwa la hamaki
Magharibi mashariki
Limeikumba dunia | 13. Zungumza kirafiki
Kwa hoja na mantiki
Kipimo bora ni hiki
Cha mtu alokomoa |
| 5. Maumivu ya hamaki
Yako kwa mwenye hamaki
Wengine hupata dhiki
Wanaomtegemea | 14. Kituo changu ni hiki
Maneno mengi sitaki
Mtnzi msitahiki
Juma mwana Magambilwa |
| 6. Yeyote mwenye hamaki
Jambo kama halitaki
Hufoka kama fataki
Badala kuelezea | |
| 7. Auguwaye hamaki
Ahisi hakubaliki
Na wala haheshimiki
Anaye dharauliwa | |
| 8. Hasara zakuhamaki
Ni nyingi hazisemeki
Kufoka na kuhamaki
Kwafanana na kichaa | 1. Kwanza nawataka hali
Mimi njema yangu hali
Kimwili na kiakili
Mitazamo na hisia |
| 9. Akiwa kwenye hamaki
Kurudi nyuma hataki
Chakula hakimezeki
Usingizi hukimbia | 2. Nilisha sema awali
Siwezi ni kakubali
Watu wapata ajali
Nikiweza nazuwia. |
| 10. Ikiondoka hamaki
Dhamiri zamshitaki
Majuto kwake hubaki
Kwa kule kushambulia | 3. Nimeiona ajali
Yajeruhi maadili
Nataka tuikabili
Ndilo nimewaitia |
| 11. Yeyote mwenye hamaki
Kwa mimi haaminiki
Sintojenga urafiki
Na mtu kama kichaa | 4. Jina la hiyo ajali
Ndilo ndumilakuwili
Joka la vichwa viwili
Hatari nawaambia |
| 12. Jambo kama hulitaki
Si vizuri kuhamaki | 5. Nataja ndumila kuwili
Hutenga watu wawili
Hadi wafike mahali
Ni kama chui na paa |
| | 6. Hali ya kuwa awali
Marafiki kweli kweli
Kapita ndumila kuwili
Kawaletea balaa. |

32. USIWE NDUMILAKUWILI

1. Kwanza nawataka hali
Mimi njema yangu hali
Kimwili na kiakili
Mitazamo na hisia
2. Nilisha sema awali
Siwezi ni kakubali
Watu wapata ajali
Nikiweza nazuwia.
3. Nimeiona ajali
Yajeruhi maadili
Nataka tuikabili
Ndilo nimewaitia
4. Jina la hiyo ajali
Ndilo ndumilakuwili
Joka la vichwa viwili
Hatari nawaambia
5. Nataja ndumila kuwili
Hutenga watu wawili
Hadi wafike mahali
Ni kama chui na paa
6. Hali ya kuwa awali
Marafiki kweli kweli
Kapita ndumila kuwili
Kawaletea balaa.

MASHAIRI YA KIJAMII

- | | | |
|-----|--|--|
| 7. | Ukiwa ndumila kuwili
Tutakupishia mbali
Tena mbali kweli kweli
Usije tuharibia. | Kimwili na kiakili
Kimawazo na hisia |
| 8. | Asubuhi ndumilakuwili
Akivaa kanda mbili
Kwenye nyumba mbali mbali
Zote atatembelea | 2. Ndugu zangu nawajali
Kwa nasaha mbali mbali
Mabaya tuyabadili
Mazuri kuyaendea |
| 9. | Jioni aenda mbali
Kwenye mtaa wa pili
Ya mtaa wa awali
Enda kuyaendeleza | 3. Nikigundua dalili
Inayotuweka mbali
Ya uhalisi wa hali
Siwezi kunyamazia |
| 10. | Uso wa ndumilakuwili
Umepigwa udhalili
Hawezi kusema kweli
Ugomvi ukitokea | 4. Nimegundua ukali
Wa vitendo na kauli
Ni dalili za akili
Changa hazijakomaa |
| 11. | Ataka ndumilakuwili
Wagombanao wawili
Wote wao wakubali
Yeye mwema wa mtaa | 5. Mwenye maneno makali
Ni mtu mwenye dosari
Hata akiwa na mali
Watu watamkimbia |
| 12. | Wagombanao wawili
Mbele ya ndumilakuwili
Hufurahi kweli kweli
Kama kapewa rupiya | 6. Kwa nini uwe mkali
Elekeza kwa dalili
Kwa kila mwenye akili
Mbona atakuelewa |
| 13. | Wakubwa wa serakali
Wakitafuta ukweli
Shahidi Ndumilakuwili
Wote atawatetea | 7. Dalili za kiakili
Mwerevu atakubali
Mpumbavu hakubali
Fanya kumpuuzia. |
| 14. | Wacha undumilakuwili
Rudi kwenye maadili
Mwisho hapa sendi mbali
Magambilwa nawambia. | 8. Jifundishe kuhimili
Unapotoa kauli
Si lazima wakubali
Uhuru kuwaachia |
| | | 9. Kuhemkwa na ukali
Ni kuoyesha dalili
Mwenyewe huji kubali
Watu wawategemea |
| | | 10. Watu wakikukubali
Wewe ni mtu mahili |

33. KUHEMKWA NA UKALI

- | | | |
|----|--|----|
| 1. | Ndugu zangu vipi hali
Mimi safi kweli kweli | 27 |
|----|--|----|

MASHAIRI YA KIJAMII

- Meno thelathi na mbili
Ndipo unapoyatoa
11. Ndugu usiwemkali
Nakuomba ubadili
Njia ziko mbali mbali
Za kidiplomasia
12. Leo sintoenda mbali
Shikeni Tangazo hili
Beti ya kumi na mbili
Magambilwa naishia.
7. Sasa huyu mlemavu
Na wewe si mlemavu
Kafanye kazi kwa nguvu
Uje kumuhudumia
8. Fikiri kwa utulivu
Uachane na uvivu
Uchukulie uvivu
Dhambi na tabia mbaya
9. Apenda mtu mwerevu
Achume kwa zake nguvu
Apate na utulivu
Pia ataheshimiwa

34. KUBWETEKA

1. Nasalimia kwa nguvu
Kwa moyo mkakamavu
Naomba usikilivu
Kwa nitayosimulia
2. Baada ya utulivu
Nikagundua uovu
Ni tabia ya uvivu
Siyo ya kunyamazia
3. Watu wengine wavivu
Nawaita wapotevu
Kujitia ulemavu
Ombo ombo watu hawa
4. Huvaa nguo chakavu
Chini kanda mbili mbovu
Na uso wake mkavu
Kuomba wapita njia
5. Nywele hataki kushevuvu
Kiumbe huyu muovu
Najitia ulemavu
Na wala haoni haya
6. Mwingine mtu mvivu
Anajiona mwerevu
Kutembeza walemavu
10. Wengine watu wavivu
Naomba muwe werevu
Kuweni wakakamavu
Mplate kujinasuwa
11. Okota vyuma chakavu
Au machupa mabovu
Ukiwa mvumilivu
Mbona utafanikiwa
12. Sio kushika kidevu
Na vidole kwenye shavu
Simama kwa ushupavu
Maisha yaendelea
13. Kubweteka ni uvivu
Kwenye vijiwe vibovu
Uhalifu na uovu
Ndipo unapozaliwa
14. Nawaaga kishupavu
Na muyashike kwa nguvu
ili muwe wakomavu
Magambilwa nawambia

35. SAMEHE UPATE RAHA

1. Nasalimu kwa furaha
Nimeamka na siha
Nawatakia furaha
Na mafanikio pia
2. Nahimiza msamaha
Ili tupate furaha
Mfundu una karaha
Kama hamjaujuwa
3. Watu wengi wanahaha
Kuitafuta furaha
Kwenye mipombe ya boha
Gongo konyagi na bia
4. Nahisi kupata raha
Ninapotoa nasaha
Jifunzeni msamaha
Tiba iliyotimia
5. Wengi watu wanahaha
Kama watoto wa mbweha
Kuitafuta furaha
Kila pembe ya dunia
6. Waitafuta furaha
Kwa porojo na mzaha
Watu wakawa majuha
Waliochanganyikiwa
7. Utaipata furaha
Kwa kupenda msamaha
Upate kuona raha
Maisha kufurahia
8. Wengi wataka furaha
Kwa vibweka na karaha
Majivuno na madaha
Kwa kweli wanakosea
9. Upole na msamaha
Tumia hii silaha
10. Visasi vina karaha
Vyauma kama jeraha
Kulipiza utahaha
Bila ya kufanikiwa
11. Vasasi vina karaha
Kulipiza utahaha
Kwa kuishiwa silaha
Rohoni ukaumia
12. Kupitia msamaha
Nzuri hii silaha
Hazina ya msamaha
Ni wewe ukiamua
13. Wanaotaka furaha
Wajifunze msamaha
Si pombe wala madaha
Yawezayo kutufaa
14. Nawaaga kwa furaha
Mungu awape furaha
Na ahaidi msamaha
Wote walonikosea

36. TUWE WABUNIFU

1. Hali zenu watukufu
Muwazima sina hofu
Nataka kuwaarifu
Kitu nimekigundua
2. Tabia ya ubunifu
Ina heshima tukufu
Na faida maradufu
Tupate kujikomboa
3. Shida za muda mrefu
Misukosuko na hofu

MASHAIRI YA KIJAMII

- | | |
|--|--|
| Kupitia ubunifu
Twaweza kuziondoa | Jina langu maarufu
Juma mwana Magambilwa |
| 4. Pasipo na ubunifu
Pamejaa usumbufu
Magonjwa na udhaifu
Ndipo yatakimbilia | 1. Namshukuru Muumba
Wetu wa hii dunia
Ni yeje nina muomba,
Amani kutupatia
Najanga limetukumba,
Wananchi Tanzania
Bara unguja na pembra,
Poleni wa Tanzania |
| 5. Kwa kuwa na abunifu
Ondowa shaka na hofu
Mawazo yenye uchafu
Fikra ziweke sawa | 2. Mwaka jana Septemba
Tarehe tisa sikia
Meli inakwenda Pemba
Unguja ikitokea
Kabla kufika Pemba
Nungwi ikadidimia
Bara Unguja na Pemba
Poleni wa Tanzania |
| 6. Kazi za muda mrefu
Zinaleta uzoefu
Changanya na ubunifu
Shida utaziondoa | 3. Abiria kwenda Pemba
Wengine wenda kuoa
Wengine wamejipamba
Wanatoka kuolewa
Wengine Wenda Pemba
mara kwanza Kupajua
Bara Unguja na Pemba
poleni wa Tanzania |
| 7. Ukiwa na ubunifu
Mwerevu mchangamfu
Kazini ukistafu
Kwako haitosumbua | 4. Kwanza meli iliyumba
Kabla kudidimia
mkatuarifu kwamba
Wenzenu twadidimia
dua nydingi Tukaomba
njia iliyobakia
Kumuachia Muumba
Apate kuwaokoa
Bara Unguja na Pemba |
| 8. Asiye na ubunifu
Akija kustaaful
Ataanza kudhoofu
Kwa kuwa na hali mbaya | |
| 9. Japo kuuza madafu
Au kuni za madifu
Hata maji ya barafu
Fanya utafanikiwa | |
| 10. Wacha mashaka na hofu
Mwenzetu umestafu
Ingawa umestafu
Maisha ya endelea | |
| 11. Jifundishe ubunifu
Pengine ukistafu
Kuna maisha marefu
Yanayo kusubiria | |
| 12. Kwaherini watukufu
Muishi muda mrefu | |

37. KUZAMA KWA MELI

1. Namshukuru Muumba
Wetu wa hii dunia
Ni yeje nina muomba,
Amani kutupatia
Najanga limetukumba,
Wananchi Tanzania
Bara unguja na pembra,
Poleni wa Tanzania
2. Mwaka jana Septemba
Tarehe tisa sikia
Meli inakwenda Pemba
Unguja ikitokea
Kabla kufika Pemba
Nungwi ikadidimia
Bara Unguja na Pemba
Poleni wa Tanzania
3. Abiria kwenda Pemba
Wengine wenda kuoa
Wengine wamejipamba
Wanatoka kuolewa
Wengine Wenda Pemba
mara kwanza Kupajua
Bara Unguja na Pemba
poleni wa Tanzania
4. Kwanza meli iliyumba
Kabla kudidimia
mkatuarifu kwamba
Wenzenu twadidimia
dua nydingi Tukaomba
njia iliyobakia
Kumuachia Muumba
Apate kuwaokoa
Bara Unguja na Pemba

MASHAIRI YA KIJAMII

- Poleni wa Tanzania
5. Analotaka Muumba
Husema Kuwa likawa
tumekesha tukiomba
Pasi na kufanikiwa
meli iliyumbayumba
Hadi ikadidimia
Bara Unguja na
Pemba poleni wa Tanzania
6. Huzuni kubwa ni kwamba
Simu mlitupigia
makelele yalipamba
kwenye meli Twasikia
nusura mkiomba
Nani wa kutuokoa
Bara Unguja na Pemba
Poleni wa Tanzania
7. Hali moto ilipamba
Nasi tukawapigia
miito ya simu yaimba
pasi na kupokelewa
Badala kufika Pemba
Kwenye maji mmeфia
Bara Unguja na Pemba
Poleni Tanzania
8. Badala kufika Pemba
Mwenyezi kawapokea
Kwa udi na kwa uvumba
Kifo Kitatufikia
uhai ni kama Kamba
mwisho hutukatikia
Bara Unguja na Pemba
Poleni Wa Tanzania
9. Twawaombea Muumba
Walokuja kuokoa
Juhudi zitapopamba
kweli watafanikiwa
- Kwa baraka za muumba
Wangali wanapumua
Bara Unguja a Pemba
poleni wa Tanzania
10. Haifai kujigamba
Wale mlookolewa
kwenye mdomo wa mamba
Chupu chupu kuponea
kawaokoa muumba
Mwenda kumtumikia
Bara Unguja na Pemba
Poleni Watanzania
11. Bara Unguja na Pemba
Tukumbuke tumefiwa
Kura msije kuomba
Vifo hivi kupidia
kura sipingi kuomba
ili kututumikia
Bara Unguja na Pemba
Poleni Watanzania
12. Bara Unguja na Pemba
Wajane tumeachiwa
Wabaki kwenye majumba
wasije kutimuliwa
Mashangazi na wajomba
Mayatima kuwalea
Bara Unguja na Pemba
Poleni Watanzania
13. Nasimamisha kuimba
Beti hii naishia
Ewe Mola twakuomba
Walokufa ghufiria
mtenzi naitwa Juma
Saidi wa Magambilwa
Bara na Unguja na Pemba
Poleni Watanzania.

38. MAFURIKO YAFIKAPO

1. Wahanga wa mafuriko, salamu nawatolea
Poleni kwa mafuriko, mali zenu kupoteka
Huo ni mzunguuko, wa maisha ya dunia
Poleni kwa mafuriko, ndugu zetu Tanzania.
2. Nasema ni mzunguko, ndugu umewafikia
Wengine si mafuriko, tetemeko hutokea
Wengine si tetemeko, kifusi kuwafukia
Poleni kwa mafuriko, ndugu zetu Tanzania
3. (3) Bila kuchapwa kiboko, kitandani anafia
Ni kokote uendako, mauti ya kufikia
Mwingine kwa mafuriko. Au kwa nydingine
njia
Poleni kwa mafuriko, ndugu zetu Tanzania
4. Ajali ikiwa yako, huwezi kuikimbia
Hata kama ngao yako, jumba lakuchomolea
Yakimkuta mwenzako, usije kushangilia
Poleni kwa mafuriko, ndugu zetu Tanzania.
5. Tukisema mafuriko, nchi nyangi hutokea
Hapa kwetu mafuriko, mara nyangi hutujia
Yaleta masikitiko, roho nyangi hypotea
Poleni kwa mafuriko, Ndugu zetu Tanzania
6. Pengine ajali yako huwezi kukimbia
Ushauri wangu kwako, pakujenga zingatia
Usijenge nyumba yako, maji yanapopitia
Poleni kwa mafuriko, ndugu Zetu Tanzania
7. Sisemi ajali yako, waweza kuikimbia
Jambo la muhimu kwako, tahadhari
kuchukua
Kwa shani za Mola wako, mbona utajiokoa
Poleni kwa mafuriko, Ndugu zetu Tanzania
8. Kukumbwa na mafuriko, Si uzembe si hatia
Moja ya misukosuko, ya maisha ya dunia
Ila tahadhari kwako, ni wajibu kuchukua
Poleni kwa mafuriko, ndugu zetu Tanzania
9. Kanuni ya Mola wako, inatueleza kuwa
Hakuna mabadiliko, wewe usipoamua
Yapange maisha yako, ndipo Mola huingia
Poleni kwa mafuriko, ndugu zetu Tanzania
10. Hutoki huko uliko, Kama usipoamua
Utabaki huko huko, Hata kwa miaka mia
Kanuni za Mola wako, hivi ndivyo zimekaa
Poleni kwa mafuriko, ndugu zetu Tanzania
11. Ninayo Masikitiko, kwa watu wenye balaa
Kupitia mafuriko, uchumi kujipatia
Kwa kuanzisha mifuko. Ikijazwa wanabwia
Poleni kwa mafuriko, ndugu zetu Tanzania
12. Muhanga wa mafuriko, Beti hii naishia
Ushauri wangu kwako, vumilia zingatia
Mimi ni mtunzi wako, Juma mwana
Magambilwa
Poleni kwa mafuriko, ndugu zetu Tanzania

39. MABOMU GONGO LA MBOTO

1. Habari gani watoto
Na walezi wa watoto
Na wazazi wa watoto
Nyote nawasalimia
2. Nakuja na mchakato
Una habari nzito
Mbagala Gongo la mboto
Maafa yametokea
3. Mbagala Gongo la mboto
Kwenye silaha nzito
Zile silaha nzito
Zilipotulipukia
4. Niliwaona watoto
Wavuka bonde na mito
Yale mabomu mazito
Yalipojilipukia

MASHAIRI YA KIJAMII

5. Yale mabomu mazito
Yalipuka kama moto
Anga ilijaa moto
Kila mtu kashangaa
6. Tumeona kama ndoto
Walemavu na watoto
Mbagala Gongo la mboto
Wajaribu wakimbia
7. Waenda huku kuzito
Waenda kule kuzito
Ilikuwa ni msoto
Vizuri ukiambiwa
8. Kutoka Gongo la mboto
Mgongoni na watoto
Mikononi na watoto
Wamama wanakimbia
9. Tumepata somo zito
Kina mama na watoto
Wanakiona cha moto
Majanga yakiingia
10. Leo ninatoa mwito
Amani ni kama pato
Ikifa kuna mazito
Bora kuikumbatia
11. Watakao washu moto
Vurugu ni jambo zito
Wakitafuta kipato
Vurugu ni jambo bayu
12. Nchi ikiwaka moto
Mfano Gongo la mboto
Kina mama na watoto
Na vikongwe waumia
13. Mbagala Gongo la mboto
Imeleta changamoto
Amani ni kama pato
Tusije kuichezea
14. Kitendo kama mtoto
Mjukuu ni majuto
Epuka haya mapito
Beti hii naishiya.

40. USIWE NA PUPA

1. Salaam zangu nawapa
Nyota mliyopo hapa
Hata wa mbali na hapa
Amani nawatakia
2. Nimerudi tena hapa
Nina kitu cha kuwapa
Umuhimu mkikipa
Mengi mtafanikiwa
3. Kuna ugonjwa wa pupa
Wengi wanatapatapa
Na hasara umewapa
Wengine umewaua
4. Mtu akiwa na pupa
Subira anaitupa
Kughushi na kuongopa
Njia anazopia
5. Mara nyingi mwenye pupa
Hukimbilia kukopa
Akitakiwa kulipa
Huona anaonewa
6. Mipango ya mwenye pupa
Maji kujaa na kupwa
Huku moyo akijipa
Kizito mtarajiwu
7. Mara nyingi mwenye pupa
Aweza kuwa kibopa
Atanunua matipa
Maelfu na mamia
8. Mitaji ya mwenye pupa
Anaweza kuitupa

MASHAIRI YA KIJAMII

- Kwa kununua mapipa
Bila faida kujua
9. Ushuru aweza kwepa
Bili za maji kukwepa
Kwa kufanikisha pupa
Zinazo muelemea
10. Ukiwa na mwenye pupa
Usumbufo atakupa
Kutaka hapa kwa hapa
Mwisho kuharibikiwa.
11. Ushauri ninawapa
Tujiepushe na pupa
Badala kuwa na pupa
Subira itatufaa.
12. Leo naishia hapa
Shikeni niliyowapa
Mtungaji hana pupa
Juma mwana Magambilwa.
5. Watu wengi huamini
Tukitoka duniani
Peponi au motoni
Maandiko hupitia.
6. Kinyume na wapagani
Wao wanachoamini
Baada ya duniani
Hakuna kufufuliwa
7. Haya makundi pinzani
Ya dini na wapagani
Anayetufaa nani
Kati ya wawili hawa
8. Asiyekubali dini
Na muumini wa dini
Tunaweka behewani
Siti moja wamekaa
9. Asiyeye amini dini
Ateremka njiani
Anayeaminini dini
Safari yaendelea

41. MWENYE DINI ATUFAA

1. Jamani habari gani
Nimerudi jukwaani
Kuna kitu cha thamani
Nilicho waandalia
2. Ni umuhimu wa dini
Kwa maisha duniani
Inasaidia nini
Kwa viumbe vyaa dunia
3. Leo nikitaja dini
Lengo langu ni imani
Baada ya duniani
Maisha kuendelea.
4. Maana hasa ya dini
Ninaicha pembeni
Wengi wanavyoamini
Humo humo napitia
10. Ukimkopesha deni
Anaye amini dini
Anajua hili deni
Mwisho wake ni mbaya
11. Atalipa duniani
Asije kwenda motoni
Anajua duniani
Vitendo vyahesabiwa.
12. Kinyume na mpagani
Akiwa madarakani
Atawakandamizeni
Motoni hatahofia
13. Mtu mwema huamini
Akhera ni maskani
Ishi vyema duniani
Pepo inakungojea

MASHAIRI YA KIJAMII

14. Nimefika kituoni
Sikubali upagani
Nachagua kwenye dini
Mtunzi ni Magambilwa.

Madhara yake makubwa
Itakutupa jazba
Gerezani kufungiwa.

42. WACHA JAZBA

1. Kina mama kina baba
Kuna jambo lanikaba
Nahesabu ni msiba
Uliyotuelemea.

2. Jambo hilo ni Jazba
Kwa wadogo na wakubwa
Wamezongwa na jazba
Wataka kunusuriwa

3. Kwa mtu mwenye jazba
Akipatwa na msiba
Pumzi zake humziba
Akashindwa kupumua.

4. Hata kula akashiba
Mtu awe na jazba
Kibao atakuzaba
Hasira zikimjia.

5. Uvumilivu ni haba
Kwa mtu mwenye jazba
Kibao atakuzaba
Hasira ikimjia.

6. Kooni atakukaba
Na pumzi zikakuziba
Kwa hasira na jazba
Anaweza kukuwa.

7. Kibaka anapoiba
Kwa mtu mwenye jazba
Atamfunga viroba
Na moto kumlipua.

8. Haifai jazba

9. Nimekuja na mkoba
Umejaajila Tiba
Na wale wenye Jazba
Leo nitawapa dawa.

10. Kwanza tujue jazba
Haiondoshi msiba
Ukikupata msiba
Kubali umetokea.

11. Unapochomwa na mwiba
Dawa kuchomoa mwiba
Kisha kutafuta tiba
Jazba haitafaa.

12. Ikikupata jazba
Fikiria mara saba
Subira itakubebe
Na kukuongoza njia

13. Hiyo dawa mujaraba
Inayoponya jazba
Kufikiri mara saba
Kabla ya kuamua.

14. Naufunika mkoba
Mwisho wa kutowa tiba
Yakukomesha jazba
Mtunzi ni Magambilwa.

43. TUIEPUKE DHULUMA

1. Kina baba kina mama, nyote nawasalimia
Kila ninapo simama, nina la kuwaambia
Tulitambue mapema, liwe zuri au baya
Tuiepuke dhuluma, dunia ikae sawa.

2. Mtu yejote lazima, apende kuthaminiwa
Ingawaje ni lazima, kuitwa muheshimiwa

MASHAIRI YA KIJAMII

- Mahali tunapokwama, nimekwishapagundua
Tuiepuke dhuluma, dunia ikae sawa.
3. Ufisadi na dhuluma, janga lililokomaa
Hayaleti mwisho mwema, katika hii dunia
Amani ikituwama, mwaweza kuiondoa
Tuiepuke dhuluma, dunia ikae sawa.
4. Ufisadi na dhuluma, ndugu nawapa usia
Hayaleti mwisho mwema, katika hii dunia
Amani ikituwama, mwaweza kuiondoa
Tuiepuke dhuluma, dunia ikae sawa.
5. Haipendezi dhuluma, vyovyote itavyokuwa
Urafiki utakoma, uadui kuingia
Ukifanyiwa dhuluma, vigumu kuvumilia
Tuiepuke dhuluma, dunia ikae sawa.
6. Watu dunia nzima, machafuko hutokea
Hutokana na dhuluma, viumbe kuhujumiwa
Tungejua dhuluma, wote tungeikimbia
Tuiepuke dhuluma, dunia ikae sawa.
7. Mungu hataki dhuluma, akaleta manabiya
Wakukataza dhuluma, japo kwa ganda la
mua
Hata punje ya mtama, mwenyewe
kurejeshewa
Tuiepuke dhuluma, dunia ikae sawa.
8. Watu wengi wanasema, Amani wahitajia
Hawafahamu dhuluma, juhudhi yaizuwia
Inapotanda dhuluma, amani haitokaa
Tuepuke dhuluma, dunia ikae sawa.
9. Baraza la usalama, la umoja wa dunia
Utulivu ni lazima, uwepo kwenye dunia
Vurugu na uhasama, muhimu kuviondoa
Tuiepuke dhuluma, dunia ikae sawa.
10. Baraza la usalama, la umoja wa dunia
Mara kwa mara lasema, mapigano jambo
baya
- Ajabu linapokwama, dhuluma kuiondoa.
Tuiepuke dhuluma, dunia ikae sawa.
11. Baraza la usalama, mtakapo dhamiria
Kudumisha usalama, katika hii dunia
Ikomesheni dhuluma, nawapa mia kwa mia
Tuiepuke dhuluma, dunia ikae sawa.
12. Nakumbushia heshima, kwa watu wote ni
sawa
Uongo mnayosema, wengi sasa wanajua
Baraza la usalama wacheni kupendelea
Tuiepuke dhuluma, dunia ikae sawa.
13. Dunia yawatazama, kwa macho ya sawa
sawa
Pakiwa na uhasama, vipi mwatusaidia
Upande mkiegama, mjuwe tunaelewa
Tuiepuke dhuluma, dunia ikae sawa.
14. Beti hii nasimama, mbele sitaendelea
Tuikomeshe dhuluma, bado nasisitizia
Mtunzi naitwa Juma, Saidi wa Magambilwa.
Tuiepuke dhuluma, dunia ikae sawa

44. HAKI ZA WANAWAKE

1. Waume na wanawake
Naomba msalimike
Mambo yenu yanyooke
Mnayoyahitajia.
2. Naomba msinichoke
Wala msihuzunike
Nataka mfaidike
Tenzi zangu kuititia
3. Mada ya aina yake
Hadharani tuiweke
Yawahuusu wanawake
Na nafasi yao pia.

MASHAIRI YA KIJAMII

4. Lazima ifahamike
Watu bila mwanamke
Maisha ukweli wake
Lazima utapotea
5. Heshima ya mwanamke
Pamoja na haki zake
Lazima vifahamike
Hii ndiyo sawa sawa.
6. Twamuona mwanamke
Akidai haki zake
Kutoka kwa mume wake
Wazazi na familia.
7. Umoja wa wanawake
Teteeni wanawake
Mipaka msiivuke.
Pua mkaangukia
8. Mwanamke akumbuke
Yeye ana mume wake
Wakati wa ndoa yake
Kakiri kutawaliwa
9. Kaapishwa mume wake
Kulipa mahali kwake
maisha ya mwanake
mume kumsimamia.
10. Akizaa mwanamke
Yeye na watoto wake
Mume ni wajibu wake
Wote kuwahudumia.
11. Ajitia mwanamke
Kutafuta haki zake
Pengine malengo yake
Yako nyuma ya pazia.
12. Mbona sasa mwanamke
Zatumika picha zake
Wanaume waburudike
Biashara kuvutia.
13. Mwanamuziki wa kike
Atembeza mwili wake
Wanaume wavutike
Uwapi huo usawa
14. Namuomba mwanamke
arudi kwa Mola wake
Atakuta haki zake
Beti hii naishia

45. AKIGOMA DAKTARI

1. Nawauliza habari
Hali yangu ni nzuri
Yenu ikiwa nzuri
Mimi nitafurahia.
2. Nakuja na mashauri
Muyatazame vizuri
Kinyume chake hatari
Yaweza kutufikia.
3. Kugoma madaktari
Duniani ni hatari
Ewe Mola tunusuru
Yasitrudie haya.
4. Kusoma udaktari
Ni uamuzi mzuri
Ukiwa na lengo zuri
Mbona utafanikiwa.
5. Nafasi ya Daktari
Katika kutustiri
Nashuhudia nakiri
Wanafaa kuenziwa.
6. Wakubwa wa jamhuri
Wabunge na mawaziri
Wahitaji daktari
Hata mabilionea.

MASHAIRI YA KIJAMII

7. Mafukara matajiri
Wakazi na wasafiri
Wahitaji daktari
Aje kuwahudumia.
8. Tumlipe daktari
Afanye kazi vizuri
Makazi na Usafiri
Na marupurupu pia.
9. Nakuomba daktari
ufanye kazi vizuri
Uzidishe uhodari
Viumbe kuwaokoa.
10. Kazi yako daktari
Mungu aona vizuri
Ifanye kwa utayari
Mbona utafanikiwa.
11. Usivuke mstari
Ukigoma ni hatari
Watakufa mawaziri
Wabunge hata raia.
12. Kaa mbali daktari
Watakutia dosari
Wanasiasa washari
Wasije kukuhadaa.
13. Haki zako daktari
Ukizijua vizuri
dai bila ujeuri
haki haitapotea.
14. Naifupisha habari
Kwa heri madaktari
Juma Saidi Nasri
Magambilwa awaambia.
2. Naukemea ulevi
Wasabisha magomvi
Ndugu zangu kwenye jamvi
Sikuja kushambulia.
3. Samahanini walevi
Mwayazua magomvi
Ndugu zangu kwenye jamvi
Sikuja kushambulia
4. Hauchagui ulevi
Mume akiwa mlevi
Japo mkewe mlevi
Vurugu litatokea
5. Mke awe ni mlevi
Mume asiwe mlevi
Watakuwa hawawivi
Vyovyote itakavyokuwa
6. Mume sasa ni mlevi
Mke wake si mlevi
Yatafumuka magomvi
Hadi watu watajaa.
7. Muumini wa ulevi
Muombe hela ya chumvi
Akunyima hivi hivi
Bora ungeomba bia.
8. Anapolala mlevi
Anakuwa mlalavi
Na kulala hivi hivi
Bila viatu kuvua.
9. Hata baba mwenye mvi
Nyingi kama chavichavi
Atashiriki ulevi
Heshima humpotea.

46. MADHARA YA ULEVI

1. Habari za sasa hivi
Na simama kwenye jamvi

MASHAIRI YA KIJAMII

10. Aweza zusha ugomvi
Na vitoto hivi hivi
Vitendo vibaya hivi
Ulevi hutuletea
11. Ndugu wacheni ulevi
Kukwepa vitendo hivi
Vichocheo vya magomvi
Tuinusuru dunia.
12. Ninakaa kwenye jamvi
Baada ya vineno hivi
Amuweni sasa hivi
Anasema Magambilwa.
13. Au kauze viepe, uvivu uuondoe
Naonya usiwe kupe, jitegemee mwenyewe.
14. Tunapomtaja kupe, ni mdudu tuelewe
Ang'ang'aniya kupe, kwenye mwili wa Nguruwe
Ataganda anenepe, katelekeza wanawe
Naonya usiwe kupe, jitegemee mwenyewe.
15. Kama hujaona kupe, kwenye mbwa na Nguruwe
Njia nyingine nikupe, kwenye Ng'ombe kakague
Hawezi kutoka kupe, japo atapigwa mawe
Naonya usiwe kupe, jitegemee mwenyewe.
16. Kufikia hapa kupe, amemganda Nguruwe
Anyonye na anenepe, hapendi aondolewe
Wala asitapetape, japo apigwe kwa mawe
Naonya usiwe kupe, jitegemee mwenyewe.
17. Naomba usiwe kupe, ni mtuhumiwa wewe
Maisha usiogope yanakusubiri wewe
Majukumu usikwepe, kila kitu ufanyiwe
Naonya usiwe kupe, jitegemee mwenyewe.
18. Mtaji nenda kakope, tulia udhaminiwe
Zungusha ukaulipe, na kesho uaminiwe
Wajinga wasijitape, na kukudharau wewe
Naonya usiwe kupe, jitegemee mwenyewe
19. Kwa moyo safi mweupe, ninakushauri wewe
Watu heshimu wakupe, sipendi upuuziwe
Na hata moyo ujipe, kwa Mungu ubarikiwe
Naonya usiwe kupe, jitegemee mwenyewe
20. Ukiishi kama kupe, wajikaanga mwenyewe
Kula shiba unenepe, sipendi upuuzike
Na hata moyo ujipe kwa Mungu ubarikiwe
Naonya usiwe kupe jitegemee mwenyewe.
21. Jipange usiogope, usingizini jitoe
Mwenyezi nini akupe, ili ushukuru wewe

47. USIWE KUPE JITEGEMEE

1. Kwanza salaam niwape, wa kwetu na kwa wengine
Kwa moyo safi mweupe , Rai zangu nizitowe
Nzuri msiogope, zitatufaa wenyewe
Naonya usiwe kupe, jitegemee mwenyewe
2. Naomba usiwe kupe, jitegemee mwenyewe
Tafuta usiogope. Lima hata njugu mawe
Kamata nyundo na Chepe, bora kupasuwa mawe
Naonya usiwe kupe, jitegemee mwenyewe.
3. Hasara ukiwa kupe, utadhalilika wewe
Kila siku uongope, ili chakula upewe
Nakujifanya mapepe , vichekesho uvitoe
Naonya usiwe kupe, jitegemee mwenyewe.
4. Jina la hovyo wakupe, chakula usimangiwe
Wakonyezane kwa kope, kila ukifika wewe
Hali hii iogope, isikufikie wewe
Naonya usiwe kupe, jitegemee mwenyewe.
5. Naonya usiwe kupe, yafaa utegemewe
Ingia kwenye matope, ukalime njugu mawe

MASHAIRI YA KIJAMII

Kwa hapa tusiogope, shairi langu
mwishowe
Naonya usiwe kupe, jitegemee mwenyewe.

Kesi itarushwa rushwa
Bila kukuhurumia
9. Na haki itapindishwa
Usipoitoa rushwa
Unaweza ukatishwa
Haki ukaikimbia.

48. MADHARA YA RUSHWA

1. Neema kwenu kushushwa
Balaa likiondoshwa
Maisha yakirefushwa
Kwa Mola nawaombea;
2. Leo nimekorofishwa
Na wanaodai rushwa
Na haki imepotoshwa
Usipo kuinunua.
3. Mtoa na mla rushwa
Wote wananuka rushwa
Wafaa kuadabishwa
Wasije wakarudia.
4. Hatari ni hii rushwa
Kama isipoondoshwa
Uchumi utaangushwa
Maadili kupotea.
5. Ukitaka kukopeshwa
Waambiwa toa rushwa
Upate kuorodheshwa
Karani akuambia
6. Cheo huwezi pandishwa
Waweza hata kushushwa
Pasipo kutowa rushwa
Nani atakusikia.
7. Polisi ukifikishwa
Hutoki bila ya rushwa
Mahabusu wabakishwa
Usipojiangalia
8. Hakimu ataka rushwa
Kataa kutoa rushwa
9. Na haki itapindishwa
Usipoitoa rushwa
Unaweza ukatishwa
Haki ukaikimbia.
10. Haiwezi koma rushwa
Kama tusiporudishwa
Kwenye dini kufundishwa
Kesho tutafufuliwa.
11. Kupitia hii rushwa
Watu wema huangushwa
Viti vyao kukalishwa
Wabovu wasiofaa.
12. Mola achukia rushwa
Na wewe chukia rushwa
Sote tukipinga rushwa
Maisha yatatalia.
13. Hakimu umeapishwa
Polisi umeapishwa
Mwiko kupokea rushwa
Mwenyezi kashuhudia
14. Na rehema itashushwa
Msamaha utashushwa
Beti hii naishia
Juma mwana Magambilwa

49. UKABILA NA UDINI

1. Ndugu mna hali gani, mimi hali yangu sawa
Leo sitokaa chini, napita kila mtaa
Nikifanya kampeni, kila pembe ya dunia
Ukabila na udini, hauleti manufaa
2. Ukabila na udini, mwenzenu nimegundua
Ni hatari maishani, napita nikikemea

MASHAIRI YA KIJAMII

- Macho yenu fumbuweni, muone mawili
haya
Ukabila na udini, hauleti manufaa.
3. Wanadamu kumbukeni, ni ndugu wa
kuzaliwa
Sote tunayo thamani, mbele ya Mungu ni
sawa
Rangi kabilia sishani, isije kuwahadaa
Ukabila na udini, hauleti manufaa.
4. Ukabila naamini, kila mtu kaelewa
Nina shaka na udini, vigumu kuuelewa
Mkemeaji udini, vibaya anadhaniwa
Ukabila na udini, hauleti manufaa.
5. Mimi nahimiza dini, udini naukemea
Nini dini na udini, vigumu kupambanua
Tofauti kubaini, yahitaji kutulia
Ukabila na udini, hauleti manufaa.
6. Dini tunavyoamini, ni mfumo au njia
Watu wanapoamini, hii ndiyo sawasawa
Wakaishi duniani, njia hiyo kupitia
Ukabila na udini, hauleti manufaa.
7. Wengine ni wapagani, Mungu wanamkataa
Ambao wanaamini hakuna kufufuliwa
Hii nayo ni imani, inaitwa dini pia
Ukabila na udini, hauleti manufaa.
8. Wengine wana amini, bila Yesu kupitia
Hata ukifanya nini, moto unakungojea
Wengine mabaniyani, wengine
Muhammadiya
Ukabila na udini, hauleti manufaa.
9. Makundi yanatamani watu wa hii dunia
wote tuwe waumini, dini yao kuingia
lengo ni kututhamini, tusije tukapotea
ukabila na udini, hauleti manufaa.
10. Hapa kosa sillioni, kama tukizingatia
Itikadi na imani, kila mtu huamua
Hailazimishwi dini hilo Mungu anajua
Ukabila na udini, hauleti manufaa.
11. Hili tukilibaini muda tutauokoa
Na kuitumia dini, wote kuwahudumia
Yahimiza kila dini, wanadamu wote sawa
Ukabila na udini, hauleti manufaa.
12. Kwa mtu mwenye udini, wengine awabagua
Wasiofuata dini, yake aliyochagua
Hawezi kuwathamini, hata wakifa kwa njaa
Ukabila na udini, hauleti manufaa.
13. Mkiendana imani, japo uwe haramiya
Jua atakuthamini, mpaka utashangaa
Na huu ndiyo udini, hata Mungu akemea
Ukabila na udini, hauleti manufaa.
14. Ukabila na udini, si moto wakuchochea
Wakurugenzi wa dini, simameni kukemea
Ujanja wenu wachenii, ndipo mtafanikiwa
Ukabila na udini, hauleti manufaa.
15. Dunia yenyé amani, ni rahisi kuchagua
Tukiishi kwa imani, sote tuna haki sawa
Nimefika kituoni, Juma mwana
Magambilwa
Ukabila na udini, hauleti manufaa.

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhangaa wa Imam Hussein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imam Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhabimi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Uduhuu kwa mujibii wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'an Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni schemu ya Qur'an na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongiza vijana wa kizazi kipyta
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherkeea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatocha changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuuy ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuuy ya Pili
63. Kuzura Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatoo
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nine

MASHAIRI YA KIJAMII

68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-lлаah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a)
83. Mazingira
84. Utokozo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgongwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'animebadilishwa
100. Idi Al-Ghadir
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kumsalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kufuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruki
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu

MASHAIRI YA KIJAMII

141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'an Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s.)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhan
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislamu wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madhehebu
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'an
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhan)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina ('as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwenendo wa Imam 'Ali ('a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kuteeta Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hijra ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhiila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (*Al-Muraja'aat*)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Mjadala wa Kitikadi
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
213. Imam Ali na Mambo ya Umma

MASHAIRI YA KIJAMII

-
- 214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
 - 215. Mwanamke na Sharia
 - 216. Mfumo wa Wilaya
 - 217. Vipi Tutaishinda Hofu?
 - 218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
 - 219. Mahali na Mali za Umma
 - 220. Nahjul-Balaghah – Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
 - 221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
 - 222. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
 - 223. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
 - 224. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
 - 225. Maeneo ya Umma na Mali Zake
 - 226. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
 - 227. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?
 - 228. Maimamu wa Ahlul Bait – Ujumbe na Jihadi

KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

- 1. Amateka Na Aba' Khalifa
- 2. Nyuma yaho naje kuyoboka
- 3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
- 4. Shiya na Hadithi.

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAHI FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSI

- 1. Livre Islamique